# Nipashe

Jumatano Aprili 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580564

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**UCHUNGUZI** tuhuma bosi TPA wasubiri ukaguzi wa CAG




UKURASA 3

**POLISI** waimarisha ulinzi mkutano Mkuu Maalum CCM

UKURASA 2

# Kicheko kushuka gharama za bidhaa kutoka Zanzibar

**Ni** matokeo ya kuzipatia ufumbuzi kero za Muungano...

*Uk. 2*



## YALIYOMO

UKURASA WA NNE

### WALALAMIKIA ARDHI YAO KWA RAIS SAMIA

WANANCHI wa Madabala na Mbwawa mkoani Pwani, wameelekeza malalamiko yao kwa Rais, Samia Suluhu Hassan, kutokana na kile wanachodai kutaka kunyang'nywa mashamba yao na...

UKURASA WA 4

### PM AONYA WATUMISHI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaonya watumishi kuacha usumbufu kwa wawekezaji wanapofika kupata ushauri kwenye ofisi zao



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, akionyesha furaha baada ya kukabidhiwa tuzo maalum na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Ally Possi (kushoto) ya kutambua mchango wake katika kukuza na kuendeleza sekta ya habari kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, wakati wa kongamano la Siku ya Uhuru wa Habari Duniani, jijini Dar es Salaam, jana. PCHA: JUMANNE JUMA

## Viongozi wanawake IPP Media wapata tuzo

UKURASA 3

# Mbatia aibua hoja Katiba Mpya

UK. 2

**MICHEZO** TSHABALALA SOKONI SH. MILIONI 392 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbatia aibua hoja ya Katiba Mpya

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amesema ipo haja ya kuwapo kwa tume huru ya maridhiano ambayo itazaa upatikanaji wa Katiba mpya, itakayotokana na wananchi.

Amesema mchakato wa upatikanaji Katiba mpya ulioanzishwa mwaka 2013 na Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete na kupatikana Katiba iliyopendekezwa bungeni, haikupatikana kwa mfumo wa wananchi.

Mbatia aliyasema hayo jana jijii Dar es Salaam, katika mahojiano maalum na Nipashe, kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo ya hali ya kisiasa nchini.

Alisema ili kufikia mwafaka wa kitaifa uliyo na umoja, inahitajika suluhu ya kisiasa kutoka kwa wananchi kupitia meza ya majadiliano.

"Zao la Katiba lilianzishwa na rais, si sawa. Pamoja na kumpongeza Kikwete kuanzisha mchakato ule, udhaifu wa mfumo wetu ulifanya rais aanzishe mchakato huo, bado ilitakiwa mchakato uanzishwe na wananchi, sababu ni ya wananchi.

"Katiba ni mama, Bunge, Mahakama, serikali ni mtoto, na rais yupo ndani ya Katiba, utaona upatikanaji wake haukuwa wa wananchi," alisema Mbatia.

Kuhusu rasimu ya Jaji Joseph Warioba, alisema inaweza kuwa ni Katiba itakayotokana na wananchi, kutokana na maandalizi yake kuhusisha maoni ya wananchi.

"Katiba hii tuliyonayo sasa ya mwaka 1977, pamoja na kufanyiwa marekebisho kadhaa, bado inaminya demokrasia na uwanja usio sawa wa kisiasa.

"Katiba inatoa haki ya kufanya siasa kwa vyama vya siasa vilivyosajiliwa, lakini wakati huohuo inapoka uhuru na haki hiyo, kwamba marufuku mikutano ya kisiasa kwa vyama," alifafanua Mbatia.


Aliongeza kwamba Katiba iliyopo sasa inatoa madaraka makubwa kwa rais na kuwateua viongozi mbalimbali ikiwamo wakuu wa mikoa, wilaya na hata wakurugenzi.

"Tume ya mabadiliko ya Katiba ni mawazo kutoka kwa wananchi, ikizingatiwa tunu za taifa, uzalendo, uadilifu, umoja na uwajibikaji, likaja bunge likagawanyika katika misingi ya kiitikadi na upande mmoja ulitengeneza Katiba iliyopendekezwa."

"Katiba iliyopo ya mwaka 1977, bado ni ya mfumo wa chama kimoja, Ibara ya 10 inatoa haki ya kuruhusu mikutano ya kisiasa lakini ina upungufu mkubwa," alisisitiza Mbatia.

Kadhalika, Mbatia alisema kuwapo kwa vyama ambavyo havina ushindani kunatokana na Katiba ambayo haitoi uhuru wa kidemokrasia kwa usawa kutokana na baadhi ya vifungu.

Alibainisha kwamba kukubalika mfumo wa vyama vingi mwaka 2010 ilikuwa ni kwa asilimia 48 hadi 50 na hivi sasa vyama vingi vinahitajika kwa asilimia zaidi ya 80.




Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi Taifa, James Mbatia, akifafanua jambo kuhusu katiba mpya, wakati wa mahojiano na gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

"Maendeleo ni watu, kurudishwa nyuma kwa vyama vya siasa katika uwanja huru wa kidemokrasia, kutokana na kuitumia Katiba hii hii, kwamba dola izuie mikutano kumerudisha nyuma juhudi za kwenda mbele.

"Vyama vya siasa sasa vinazungumzia udini, ukabila, kutokana na kukosa hoja imara za kisiasa, fikra zimerudi nyuma hakuna kufikiri shughuli za msingi katika kulijenga taifa."

Akizungumzia serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan, alisema ikitoa fursa ya uhuru wa vyombo vya habari, haki na demokrasia kutaifanya nchi kusonga mbele.

"Hivi sasa vyombo vya habari ndio kila kitu. Media ni bidhaa ghali zaidi duniani naweza kusema ni taarifa, sababu inatoa taarifa za mahali popote na taarifa ni maendeleo, unapominya uhuru inaathiri kila kitu."

Alisema pamoja na hotuba za Rais Samia kugusia masuala mbalimbali ambayo yanarudisha demokrasia nchini, akumbuke suala la jinsia kwenye nyadhifa tofauti za uongozi.

"Kwa namna gani rais anashawishi wanawake na wasichana katika uongozi, iwe rejea kwa bara la Afrika, sauti za uhuru wa kifikra zikasikika."

**■Usikose kufuatilia mahojiano kwa upana kesho**

# Maandalizi ya mkutano mkuu wa CCM usipime

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAANDALIZI ya vikao vikubwa vya Chama cha Mapinduzi(CCM), yamepamba moto, bendera zikiwa zimepambwa kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma, huku nyumba za kulala wageni zikijaa kuanzia kesho.

Kwa upande wake, Jeshi la Polisi limejipanga kuimarisha ulinzi katika vikao hivyo na kuwaonya watu watakaojitokeza kufanya uhalifu wa aina yoyote.

Vikao hivyo vinavyotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki hii, lengo ni kumchagua Rais, Samia Suluhu Hassan kuwa Mwenyekiti wa chama hicho.

Nipashe imezunguka katika barabara mbalimbali na kushuhudia bendera za chama hicho zikiwa zimepambwa kwenye barabara na kwenye mzunguko wa barabara, huku nyumba za kulala wageni katikati ya Jiji la Dodoma zikiwa zimejaa kuanzia kesho hadi Jumamosi.

Akizungumza kuhusu maandalizi ya vikao, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema mkutano mkuu maalum utafanyika kesho na utatanguliwa na kikao cha Kamati Kuu ya CCM Taifa na NEC.

"Maandalizi ya mkutano mkuu yamekamilika, nawakaribisha wajumbe wote Dodoma, kwenye mkutano huu ambao pamoja na mambo mengine una lengo moja kuu la kumchagua kwa kura zote za ndio Mwenyekiti wa CCM Taifa," alisema.

### KAULI YA POLISI

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, alionya makundi ya kihalifu ambayo yatajitokeza katika kipindi hicho cha mkutano huo, na kwamba jeshi hilo limejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwapo wakati wote.

Muroto alisema jeshi hilo limejipanga kuhakikisha wageni wote wanaoingia kwa ajili ya mkutano huo wanakuwa salama na kwamba kwa kushirikiana na CCM wameandaa vitambulisho maalum kwa ajili ya kuingia kwenye mkutano huo.

# Kicheko gharama mizigo toka Zanzibar

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

HATIMAYE gharama za kushusha mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayotoka Zanzibar, zimepunguzwa.

Kushushwa kwa gharama hizo ni moja ya hatua za kuzipatia ufumbuzi na kuziondoa hoja tano za Muungano ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kwa muda na wananchi wa pande zinazohusika na Muungano.

Hoja zingine ambazo zimeshasainiwa na kuondolewa ni ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwenye masuala ya kimataifa na kikanda, ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Selemani Jafo, alitoa taarifa hiyo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2021/21. Waziri Jafo alisema: "Kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kilifanyika Dodoma Julai 6, mwaka jana kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kilichofanyika Dodoma, Februari 9, 2019."

"Kikao hicho kilishauri kifanyike kikao cha kusaini hati za hoja tano ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi ili ziondolewe kwenye orodha ya hoja za Muungano," aliongeza. Alisema ofisi yake iliratibu kikao cha kusaini hati za hoja hizo za makubaliano ya kuondoa hoja za muungano zilizopatiwa ufumbuzi kwenye orodha ya Hoja za Muungano, kwamba kikao kilifanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, Oktoba 17, 2020.

Pia, alisema zipo hoja saba ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi na zinasubiri kupata ridhaa ya kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

Alizitaja hoja hizo kuwa ni tatizo la usimamizi wa ukokotoaji na ukusanyaji wa kodi kwenye huduma za simu unaofanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), changamoto za uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar.

Zingine ni kuchelewa kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete, kuchelewa kusainiwa kwa mkataba wa Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Uvuvi kwenye ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu, Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani za Kodi (TRAT) kutoka Zanzibar.

Wakichangia hoja ya kuondoa gharama za kushusha mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, kwa mizigo inayotoka Zanzibar, baadhi ya wabunge walipongeza hatua hiyo.

Mbunge wa Mtoni, Abdul Idris Juma, alisema wananchi wa Zanzibar wanapokuja Bara kusalimia ndugu zao wakiwa wamebeba bidhaa kama vile sukari yenye uzito wa kilo tano, hutozwa ushuru.

Alisema hali hiyo inatenganisha undugu uliopo baina ya pande mbili za Muungano kwa sababu asilimia 70 ya wakazi wanaoishi Zanzibar wana ndugu zao Bara.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Spika wa Bunge, Job Ndugai, ambaye alimtaka Waziri Jafo kuliangaliza vizuri.

Spika Ndugai alisema: "Hili suala la bidhaa zinazotoka Zanzibar kutozwa kodi hebu liwekeni sawa. Haya mambo ya kilo mbili za sukari kwa nini yasiwekwe sawa? Hayo mambo yamesemwa sana humu bungeni miaka nenda rudi, waziri yaondoeni ila hatujui kama bado yapo."

**HABARI KITAIFA**

# Viongozi wanawake IPP Media wapata tuzo

**Na Mwandishi wetu**

WAFANYAKAZI watatu wa IPP Media ni miongoni mwa wanawake 25 waliopewa tuzo maalum kutambua mchango wao katika kukuza na kuendeleza sekta ya habari kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

Tuzo hizo zilitolewa jana Dar es Salaam, katika halfa iliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa, Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Wanawake hao ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile na Meneja Vipindi wa EATV, Lidya Igarabuza.

Tuzo hizo zimetolewa kuelekea maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ambayo kaulimbiu ya mwaka huu ni Habari kwa Manufaa ya Umma.

Akizungumza kabla ya kutoa tuzo hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Ally Possi, alisema serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kukuza na kuendeleza sekta hiyo.

Dk. Possi alisema jukumu la wadau wa habari ni kuhakikisha wanatoa mapendekezo yatakayowezesha wanawake wanahabari viongozi kupata fursa katika nafasi mbalimbali kwenye vyombo vya habari na kuhakikisha mapendekezo yanaleta mafanikio ikiwamo kuaminiwa na wamiliki wa vyombo vya habari.

"Natoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha wanaendesha taaluma ya habari kisasa na kutumia teknolojia inayoendana na dunia ya sasa, kuwashirikisha wanawake," alisema.

Pia aliwaambia wamiliki wa vyombo vya habari kuwa wanawake wanaweza na kwamba serikali inatambua na kuthamini jitihada za kukuza na kuendeleza sekta ya habari nchini.

Kwa mujibu wa Dk. Possi, uhuru wa habari unakwenda na haki ya kupata taarifa na kwamba nchi ina sheria, katiba na mikataba ya kimataifa ambayo imeridhiwa na inaonyesha Tanzania inaheshimu na kuthamini uhuru wa habari.

"Tunaendelea kusajili vyombo vya habari kwa wingi na vinaendelea kufanyakazi, vyombo vya habari vitambue katika kupata haki na uhuru kuna wajibu. Nawasihi wamiliki wa vyombo vya habari kama mhimili wa nne kwa hiyo kalamu yetu, maneno yetu tuyatumie vizuri ili yaendeleze kujenga nchi," alisema na kuongeza:

"Uhuru wa vyombo habari una faida nyingi kama kiuchumi, kutoa elimu na tumeona wakati wa COVID 19, ajira na kuendeleza mila na desturi nchini, ni jukumu kubwa ambalo kama nchi hatuwezi kuliacha tutaliendeleza."

Aidha, alisema lazima vyombo vya habari vitumike vizuri na siyo kuharibu jamii, mila na kwamba ni muhimu kuangalia namna vyombo vya habari vinavyomtambulisha mwanamke kwamba ni kwa sura au kwa kazi anazozifanya na mchango wa kazi zake katika jamii.

Mambo ya msingi yaliyojadiliwa ni kuthamini habari na uhusiano wake kwa umma, vyombo vya habari vinavyoweza kuandaa na kutangaza maudhui nzuri, sheria za habari zinavyotekelezwa ipasavyo.

Mengine ni kutoa suluhisho la kuwezesha wanawake kushika nafasi za uongozi, ubaguzi wa ujinsia, chanzo cha unyanyasaji na jukumu la wamiliki kuongeza idadi ya viongozi wanawake.

# Uchunguzi tuhuma bosi TPA wafika pazuri

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imesema inasubiri asilimia mbili ya ukaguzi maalum kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), juu ya tuhuma zinazomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Deusdedit Kakoko.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema tayari walishakamilisha uchuguzi wao kwa asilimia 98 dhidi ya tuhuma zinazomkabili Kakoko.

"Nilishatoa taarifa kwamba tayari kwa upande wetu tulishakamilisha uchunguzi wetu. Asilimia mbili zilizobaki ni 'special audit' (ukaguzi maalum) inayofanywa na CAG. Kwa hiyo tunasubiri tuletewe hiyo iliyobaki ili tupeleke jalada kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP)," alisema.

"Sisi tunafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi nyingine na hatuwezi kupeleka jadala kwa DPP bila taasisi tunazoshirikiana nazo kutuletea sehemu yao. Baada ya CAG kutuletea, tutapeleka kwa DDP kwa sababu yeye ndiye mwenye mamlaka ya kumfikisha mahakamani kulingana na atakavyoona kwenye uchunguzi," alisisitiza.

Kakoko alishikiliwa na TAKUKURU Machi 30, mwaka huu, kwa ajili ya mahojiano dhidi ya tuhuma zinazomkabili za ubadhilifu wa zaidi ya Sh. bilioni tatu katika mamlaka hiyo.

Kakoko alisimamishwa kazi na Rais, Samia Suluhu Hassan, Machi 28, mwaka huu, baada ya kupokea ripoti mbili za CAG na TAKUKURU za mwaka 2020/2021 ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo. Baadaye nafasi yake ilichukuliwa na mtu mwingine.


ITV

USIKOSE KUFUATILIA TAMTHILIA YA

UZALO




KUANZIA 3/05/2021 SAA 1:30 USIKU

Ni tamthilia kali, yenye msisimko wa kipekee kutokea Afrika Kusini ikisheheni waigizaji mahiri kama Leleti Khumalo aliyeigiza filamu ya Sarafina.
Watoto wawili wachanga wanabadilishwa vitanda na wahudumu wa hospitali na kila mzazi kupewa mtoto asiye wake bila kujua.
Familia hizi moja ikiongoza genge la uhalifu mkubwa nayapili ikitumikia kanisa zinakuja kuwa na uadui mkubwa baada ya suala la watoto hawa kugundulika.


**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA INVENTURE MOBILE TZ LIMITED**

**Cheti cha Usajili No. 116266**

Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni Inventure Mobile Tz Limited, yenye usajili namba 1216266 kitakachofanyika tarehe 15 June 2021 ofisini kwa mfilisi saa 4:00 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi | **JOSEPH LYIMO** |
| Amwani ya Mfilisi | **PricewaterhouseCoopers Limited, Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay. P.O. Box 45. Dar es Salaam. Tanzania** |
| Tarehe ya kuchaguliwa | **10 Octoba 2020** |
| Amechaguliwa na | **WAMILIKI WA KAMPUNI** |

**Sahihi** ........................................ **Tarehe: 15 Aprili 2021**

ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS

**Jina: JOSEPH LYIMO**

**Imetolewa na;**

**JOSEPH LYIMO**

**INVENTURE MOBILE TZ LIMITED**

# Askofu awajia juu wanaobeza wanawake

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Dk. Barnabas Mtokambali, amekemea Watanzania na Waafrika wanaoendekeza desturi potofu za kudharau mwanamke na kumuona kuwa hawezi kuwa kiongozi.

Askofu huyo alisema hayo kwenye ibada maalum ya kuwasimika viongozi wakuu wa kanisa hilo, wakiwamo maaskofu na wachungaji katika kanisa la T.A.G Upendo Revival Christian Center, Area D jijini Dodoma.

Askofu Mtokambali alisema kuwa Tanzania imepata bahati ya kuwa na Rais mwanamke ambaye amepatikana kwa mujibu wa Katiba ya nchi pamoja na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ambaye naye hakuwa na matarajio ya kupata nafasi hiyo.

Akimzungumzia Rais Samia Suluhu Hassan, alisema ni kiongozi anayeweza kuongoza kwa kuwa ana uwezo, na elimu ya uongozi, ni mwenye kuwa na familia imara, lakini kutokana na tabia ya desturi za Kitanzania na Kiafrika wapo watu bado wana mtizamo finyu wanaodhani mwanamke hawezi kuongoza. "Ninawakemea watu wote waliopo Tanzania na walioko nje ya Tanzania, kuacha tabia hiyo ya kufikiri kuwa mwanamke hawezi kuongoza badala yake wanatakiwa kutambua na kuamini kuwa mwanamke anaweza kufanya kazi kubwa kama alivyo sasa Rais Samia," alisema.

Aliwataka Watanzania kuhakikisha wanaliombea taifa pamoja na kuwaombea viongozi wa ngazi ya juu wakiwamo Rais Samia, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, pamoja na baraza la mawaziri ikizingatiwa kuwa viongozi hao kufanya kazi katika kipindi ambacho hawakuwa tayari kushika nafasi hizo.

"Kwa sasa Rais Samia anaongoza huku akijipanga kutokana na kuwa hakuwa tayari kushika nafasi hiyo pamoja na makamu wa Rais hakuwa tayari kwa maana hiyo wanafanya kazi huku wakijipanga kuona wanaendelezaje yaliyopo na kuzalisha maono mapya.




Baadhi ya wafanyabiashara wa kituo cha daladala Ngamiani, jijini Tanga, wakihamisha vifaa vyao baada ya vibanda vyao vya biashara kukumbwa na bomoa bomoa, ambapo inadaiwa baadhi ya nyumba hizo zilikuwa na migogoro mahakamani. **PICHA BONIFACE GIDEON**

# Walalamikia ardhi yao kwa Rais Samia

**Na Faustine Feliciane,** KIBAHA

WANANCHI wa Madabala na Mbwawa mkoani Pwani, wameelekeza malalamiko yao kwa Rais, Samia Suluhu Hassan, kufuatia kile wanachodai kutaka kunyang'anywa mashamba yao na mwekezaji, Abdallah Saggaf, ambayo wamekuwa wakiyalima kwa zaidi ya miaka 30.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, kwa niaba ya wananchi hao, Ally Kawanda, alisema kuwa suala lao la mashamba yenye ukubwa wa heka 561 kama inavyodaiwa na mwekezaji limefika mpaka ngazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba Kata ya Visiga Wilaya ya Kibaha, lakni alishindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki wake.

"Tunamwomba Rais wetu kuliangalia tatizo letu ikiwezekana kuwaagiza wasaidizi wake wachukue uamuzi halali na haki itendeke, huyu mwekezaji alitufungulia kesi kwenye baraza la kata mwaka 2010, akidai maeneo haya ni ya kwake na alinunua kwa kutoka kwa Said Sinaela, lakini alipoombwa kuleta vithibitisho hakufanya hivyo, lakini kufika mwaka 2011 tulifunguliwa kesi Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi na bwana aliyejitambulisha kwa jina la, Hashim Saggaf, lakini na yeye alishindwa kutokea mahakamani kwa kipindi cha miaka miwili," alisema Kawanda.

Aidha mkulima na mkazi wa kijiji hicho, Anastazia Emmanuel na Abdallah Karunga, walisema Saggaf alifika kwenye kijiji hicho akiwa ameongozana na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya, Asumpta Nshama, ambaye aliwataka wananchi hao kuachia mashamba hayo kwa kuwa wamevamia eneo la muwekezaji huyo anayetaka kuuza viwanja.

"Tunaomba haki itendeke, tumekaa hapa na kuendelea na shughuli zetu za kilimo kwa zaidi ya miaka 30, leo mtu mmoja ambaye ana nguvu ya pesa anataka kututoa, tunamuomba Rais au hata Waziri wa Ardhi atusaidie ili haki itendeke," alisema Anastazia.

Alisema Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amejitahidi kutoa ushirikiano kwao, lakini wasaidizi wake wamekuwa sehemu ya tatizo hilo.

"Tarehe 10 mwezi huu wa nne mwaka 2021, Kamishna wa Ardhi Kanda ya Dar es Salaam alifanya mkutano nje ya eneo la mgogoro na alikutana na watu ambao siyo wahusika na kutoa uamuzi wa kumkabidhi eneo Saggaf, sisi hatukujua jambo hili," alisema Abdallah Kurunga.

Hata hivyo, kwa upande wa serikali kupitia kwa Kamishna wa Ardhi Kanda ya Pwani, Lucy Kabyemera, alisema suala hilo lilishamalizwa ambapo kisheria eneo hilo ni la mwekezaji Saggaf.

"Tulienda eneo la mgogoro tukiwa na Mkuu wa Wilaya na wananchi tuliwaeleza wazi kuwa eneo hilo ni la mwekezaji ambaye amekuwa akilimiliki tangu mwaka 1989, lakini tumekubaliana na mwekezaji atenge maeneo kwa ajili ya wananchi hao ukubwa wa heka 100 na sio kuwafukuza, lakini pia alitakiwa kutenga maeneo ya huduma na suala hilo kwa sasa limebaki kwenye kupima tayari kuwakabidhi wananchi," alisema Lucy.

Aidha, alisema wananchi hao kama watataka vithibitisho wanapaswa kufika kwenye ofisi yake watakapoelekezwa na kufahamishwa uamuzi uliofanyika tangu mwaka 2018.

Eneo hilo linalolalamikiwa lina ukubwa wa heka 561 ambapo mwekezaji huyo amepanga kupima viwanja na kuviuza kwa wananchi pamoja na kuweka miundombinu mbalimbali.

# PM aonya watumishi kuhusu wawekezaji

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ametoa onyo kwa watumishi kuacha usumbufu kwa wawekezaji wanapofika kupata ushauri kwenye ofisi zao badala yake wawatie nguvu ili waendelee kuwekeza.

Majaliwa aliyasema hayo alipotembelea kiwanda cha kuunganisha mabasi cha kampuni ya BM Motors kinachomilikiwa na mwekezaji Jonas Nyagawa, kilichopo eneo la Zegereni, Kibaha.

Alisema watumishi wanatakiwa kubadilika kuacha kuwasakama wawekezaji wanaofika kwenye ofisi zao na wanatakiwa kujikita kutoa huduma katika mazingira yasiyoonyesha kiashiria cha rushwa.

"Serikali yetu inayoongozwa na mama Samia Suluhu Hassan, tunasisitiza kuwa na mazingira wezeshi kwa wawekezaji na rais amedhamiria, ametoa maelekezo kila mwekezaji ambaye ameonyesha nia ya kuwekeza asibughudhiwe," alisema.

Waziri Mkuu alisema taasisi wezeshi zote zinatakiwa kuhakikisha zinatoa huduma kwa gharama nafuu kwa mazingira rahisi yasiyo na kiashiria cha rushwa.

Alisema serikali inawalinda wawekezaji wa ndani ili bidhaa zinazozalishwa zipate soko la ndani na nje ya nchi, na kinachotakiwa kwao ni kuweka malengo.

"Serikali tuko na nyie tumejenga mazingira wezeshi ya kuwekeza tunapita kusikiliza changamoto za kila mmoja na tunazitafutia ufumbuzi, nawasihi pia katika kupata mitaji tumieni benki zetu kukopa," alisisitiza.

Akizungumzia suala la kodi, Majaliwa alisema serikali imejipanga kukusanya na kwamba wameshakaa na watendaji wa Mamlaka ya Mapato (TRA) na kuwaagiza kutumia njia za kisheria kukusanya kodi.

Katika suala la ajira alisema, mpango wa nchi kuondoa tatizo la ajira ni pamoja na ujenzi wa viwanda na maeneo ya wawekezaji ni fursa pia kwa watu wengine kufungua biashara ikiwamo ya mama lishe.

Alipongeza uwekezaji unaoendelea katika mkoa huo huku akimtaka Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, kuandaa maonyesho ya bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vya mkoa huo.

Waziri Mkuu alimtaka pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa Kibaha, Jenifa Omolo, kutangaza eneo la uwekezaji na watendaji wake waondoe urasimu kwa wawekezaji wanaowatembelea.

"Halmashauri ya mji mna fursa nzuri ya kuwa na wawekezaji, enndeleeni vizuri, wito wangu ni wawekezaji kufika Zegereni kujenga viwanda.

"Tarura hakikisheni ujenzi wa barabara zote zinazokuja viwandani unaanza mara moja kwa kiwango cha lami kurahisisha magari yanayokwenda kwa wawekezaji yanapita bila shida," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alisema kiwanda hicho cha kuunganisha mabasi ni kati ya viwanda vikubwa katika mkoa huo.

Ndikilo alisema katika eneo la viwanda la Zegereni, zilikuwapo kero tatu ya maji, barabara na umeme ambazo kila mmoja imeanza kutafutiwa ufumbuzi na taasisi husika kwa ajili ya kuendelea kutoa mvuto wa wawekezaji kufika katika eneo hilo.

# TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC

*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2021
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 9,949 | 11,959 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 29,636 | 13,900 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 25,850 | 22,770 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 84 | 17,178 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 46 | 40 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 17 | 26 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 73,572 | 77,703 |
| 12 | Mali Nyingine | 11,844 | 11,310 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 18,766 | 14,813 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **169,803** | **169,739** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 909 | 1,511 |
| 18 | Amana za Wateja | 118,324 | 118,304 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 1 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,047 | 3,075 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 8,220 | 8,192 |
| 27 | Dhima Nyingine | 12,748 | 9,478 |
| 28 | Madeni | 679 | 713 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **143,928** | **141,274** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **25,875** | **28,465** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 22,543 | 10,984 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,634) | (5,627) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (2,604) | 0 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,571 | 23,108 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,875** | **28,465** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 83 | 102 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 15,488 | 11,924 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 8,352 | 6,927 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.2% | 16.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 18.6% | 15.5% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68.5% | 69.4% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 49.1% | 45.9% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 58.6% | 59.2% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.5% | 8.5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.0% | 0.2% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2021
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-21 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 6,019 | 6,551 | 6,019 | 6,551 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,172) | (1,683) | (2,172) | (1,683) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **3,847** | **4,868** | **3,847** | **4,868** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,438) | (123) | (1,438) | (123) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,152** | **1,317** | **1,152** | **1,317** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 63 | 73 | 63 | 73 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 768 | 998 | 768 | 998 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 320 | 246 | 320 | 246 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,166)** | **(6,439)** | **(6,166)** | **(6,439)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,103) | (3,315) | (3,103) | (3,315) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (3,063) | (3,124) | (3,063) | (3,124) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(2,604)** | **(378)** | **(2,604)** | **(378)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2,604)** | **(378)** | **(2,604)** | **(378)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(2,604)** | **(378)** | **(2,604)** | **(378)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 413 | 425 | 413 | 425 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (116) | (34) | (116) | (34) |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -6.1% | -1% | -6.1% | -1% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -38.3% | -7% | -38.3% | -7% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 123.3% | 104% | 123.3% | 104% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 14.2% | 18% | 14.2% | 18% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31.03.2021
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (2,604) | (8,301) | (2,604) | (378) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Hasara Katika Mali | 630 | 7,630 | 630 | 764 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 4,132 | 2,086 | 4,132 | 3,178 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (581) | 9,874 | (581) | 1,355 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (3,080) | 2,680 | (3,080) | 1,500 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (960) | 351 | (960) | (6,990) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (535) | (10,855) | (535) | (351) |
| | - Kodi Iliyolipwa | 0 | (1,877) | 0 | (416) |
| | - Mengineyo (bainisha) | (127) | 1,704 | (127) | (196) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(3,125)** | **3,292** | **(3,125)** | **(1,532)** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (76) | (133) | (76) | (46) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | (19) | 0 | (0) |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(76)** | **(152)** | **(76)** | **(46)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 16,992 | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | (0) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | (390) | (2,497) | (390) | (695) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(390)** | **14,495** | **(390)** | **(695)** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (3,591) | 17,635 | (3,591) | (2,273) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 36,259 | 18,624 | 36,259 | 18,624 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **32,668** | **36,259** | **32,668** | **16,351** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.03.2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(5,626,989)** | **3,683,694** | **0** | **16,992,072** | **28,465,109** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (2,604,317) | 0 | 0 | 0 | (2,604,317) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Miamala na wanahisa | 11,558,454 | 5,448,237 | 0 | 0 | 0 | (16,992,072) | 14,620 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (7,158) | 7,158 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.03.2021** | **22,542,870** | **7,880,154** | **(8,238,464)** | **3,690,852** | **0** | **(0)** | **25,875,413** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **0** | **0** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (377,607) | 0 | 0 | 0 | (377,607) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,897,906) | 1,636,901 | 0 | 0 | (261,005) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.03.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **2,412,126** | **4,923,845** | **0** | **0** | **20,752,304** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2021

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

***Jina na Cheo*** ***Saini*** ***Tarehe***

Juliana Swai
**(Kaimu Mtendaji Mkuu)**

Bertha Simon
**(Mkuu wa Fedha)**

Chemo Mutani
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

***Jina*** ***Saini*** ***Tarehe***

1. Ernest Massawe
2. Dr. Josephat Daniel Lotto

**Sasa unaweza kulipia malipo yote ya Serikali (GePG) na Kodi za TRA kupitia Akiba Mobile na Matawi yetu yote ambayo hayana foleni."**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maagizo ya waziri kwa TANESCO yasimamiwe

**WAZIRI** wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewataka mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme ili kufikia vijiji vyote mwaka 2022.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki, akisema kama kuna watumishi wanaoona hawataweza kukamilisha kazi hiyo kujiondoa wenyewe kabla ya kuchukuliwa hatua.

Waziri huyo alipiga marufuku mgawo wa umeme na ukataji wa umeme bila kutoa taarifa kwa wananchi na kwamba kuanzia sasa ambaye hatatoa taarifa atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Maagizo yote mawili yamekuja katika wakati mwafaka kwa kuwa siku za hivi karibuni mgawo wa umeme ulianza na hakukuwa na taarifa, kiasi cha maeneo mengi nchini kukosa nishati hiyo.

Ilianza kwa mitaa michache au umeme kukatika na kurudi kwenye nyumba chache, huku nyingi zikiachwa bila nishati hiyo kwa muda mrefu, na mbaya zaidi hakuna taarifa kwa wananchi jambo lililowafanya wengi kuathirika.

Matumizi ya majenereta yalirejea na hakukuwa na taarifa za mara kwa mara la suala hilo, huku wataalam waliojitokeza walidai kuna hitilafu ya umeme, lakini kwanini hawakutoa taarifa kwa umma ili kuwe na maandalizi hakukuwa na jibu.

Ni muhimu sana kwa TANESCO ambalo ndilo shirika pekee la kuzalisha na kusambaza nishati hiyo likaimarisha kitengo chake cha mawasiliano kuanzia ngazi ya wilaya na kutumia vyema mitandao ya kijamii katika kusambaza taarifa hizo, kuliko kusubiri taarifa zote kutolewa makao makuu.

Miaka miwili nyuma lilikuwa ndilo shirika pekee linalotoa taarifa kwa umma mara kwa mara kupitia mitandao ya kijamii ambazo zilisambaa haraka, lakini utaratibu huo ulisitishwa na hadi sasa kasi ya kutoa taarifa imepungua, jambo ambalo tunaona bado linatakiwa kufanyiwa kazi ili kurudisha utaratibu wa utoaji taarifa kwa umma.

Jingine ni kuunganisha umeme, bado kuna wananchi wengi wa mjini na vijijini wameshapeleka maombi ya kuunganishiwa umeme, lakini hadi sasa hawajapata huduma hiyo.

Sababu kubwa inayotolewa ni vifaa au danadana nyingine ambazo hazina sababu, huku wanaoumia zaidi ni wale ambao kuunganishwa kwao kunahitaji nguzo kwa kuwa hilo eneo hakua miundombinu kabisa.

Ni muhimu sana TANESCO ikatekeleza kwa kasi uunganishaji wa umeme, kwa kuwa wakati mwingine inashangaza iweje watu wa mjini ambako kuna miundombinu wanaomba kuuganishiwa nishati hiyo.

Kubwa zaidi ni kukatika kwa umeme bila taarifa ambako kumaathiri wengi kwa mali zao kuharibika, kushindwa kufanyakazi hasa wale ambao wanategemea nishati hiyo na hawana majenereta.

Nishati ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi, ni muhimu sana ikapatikana kila wakati, vinginevyo ni kukwamisha. Kama kuna matatizo ya msingi, ni vyema yakafanyiwa kazi ipasavyo ili wananchi wapate umeme kila wakati.

Tunaona kwamba maagizo ya Waziri Kalemani kwa TANESCO utekelezaji wake unawezekana kabisa, isipokuwa kinachoweza kukwamisha ni usimamizi wake.

Maagizo haya si mapya kutolewa na waziri hiyo kwa mameneja wa mikoa, lakini haijulikani ni sababu zipi zimesababisha yasitekelezeke. Aliwahi kusema kuwa kama umeme utakatika kwenye maeneo yao bila sababu maalum watawajibishwa.

Tinashauri kwamba usimamizi wa maagizo hayo uwepo, kwa kuwa watendaji wengi wa shirika hilo wamekuwa wakifaqya kazi kwa mazoea. Bila hivyo, kero kwa watumiaji wa umeme hazitaisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wasiorejesha mikopo hii wanakwamisha maendeleo

Na Beatrice Moses

**RIPOTI** ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2019/2020 iko hadharani baada ya taasisi hiyo kukamilisha

jukumu hilo la kikatiba Machi, mwaka huu na kuifikisha bungeni.

Ukaguzi ni maelekezo ya kikatiba na kwa mujibu wa ibara ya 143 (4) ya katiba ya Tanzania CAG inatakiwa kuwasilisha ripoti za ukaguzi za kila mwaka kwa Rais kabla au ifikapo Machi 31.

Kwa mujibu sheria ya ukaguzi, ripoti hizi zinakuwa tayari kwa matumizi ya umma zinapowasilishwa bungeni na wajibu huo ulifanyika ndani ya bunge jijini Dodoma.

Miongoni mwa mambo yaliyobainishwa katika tipoti hiyo ni pamoja na kuwapo mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu isiyorejeshwa ikifikia Shilingi bilioni 27.790 47.

CAG alibainisha kuwa alikagua mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 June 2020 katika halmashauri 130 na kubaini mikopo kiasi hicho bado haijarejeshwa, hali ambayo inaonyesha kwamba halmashauri husika hazikufuatilia kwa ukaribu marejesho ya mikopo kutoka kwa vikundi kulingana na makubaliano.

Taarifa hii ni mbaya hasa kwa vikundi vingine vya wanawake ambavyo vimekuwa vikisotea kupata mikopo hiyo, lakini wamekuwa wakiambulia kupigwa kalenda za kufuatilia mikopo hiyo.

Ni wazi kuwa ucheleshwaji wa mikopo hiyo ni hatua ya kuongeza kasi ya mzunguko wa ukopaji kwa vikundi vyenye sifa, ambavyo wahusika wakipata fedha hizo wenye malengo watazitumia katika kukuza mitaji yao, hivyo kupata fursa ya kujikwamua kiuchumi.

Kucheleweshwa ama kusuasusa kwa urejeshwaji wa mikopo hiyo ni kukwamisha kutekelezwa kwa ahadi za serikali, pia jitihada za wanaotarajia kukopa ambao wangefanikiwa kukuza mitaji yao wataongeza idadi ya walipa kodi.

> **Ni muhimu sana kwa TANESCO ambalo ndilo shirika pekee la kuzalisha na kusambaza nishati hiyo likaimarisha kitengo chake cha mawasiliano kuanzia ngazi ya wilaya na kutumia vyema mitandao ya kijamii katika kusambaza taarifa hizo, kuliko kusubiri taarifa zote kutolewa makao makuu.**

Katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/21), imebainishwa kuwa pamoja na malengo mengine, unakusudia kuweka mazingira wezeshi kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kujiajiri na kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Jambo ambalo wakopaji wanatakiwa kufahamishwa na kukumbushwa ni kuwa mikopo hiyo isiyo kuwa na riba haitolewi kama sadaka bali ni mkakati maalum uliowekwa kuitoa kwa gharama na masharti nafuu kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Katika kutekeleza mkakati huo, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2018 ili kuweka masharti kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya wanawake.

Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitunga kanuni zinalibaainisha masharti ya utoaji wa usimamizi wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa vikundi hivyo.

Kanuni hizo zimeainisha matumizi ya fedha za mkopo huo zinapaswa kutumika kwa miradi iliyoidhinishwa na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Mipango na Uongozi kwa kuzingatia ushauri na mapendekezo ya timu ya menejimenti na kamati ya huduma za mikopo.

Kuhusu urejeshwaji wa mkopo huo imeainishwa kuwa kila kikundi kilichopata mkopo kitatakiwa kuurejesha baada ya miezi mitatu tangu siku ya kupata fedha hizo. Inapaswa marejesho ya mkopo kufanyika kila mwezi kwa kuzingatia viwango vilivyokubaliwa kati ya mamlaka ya serikali za mitaa na kikundi kilichopatiwa mkopo husika.

Ni vyema viongozi husika wakachukua hatua za dhati kufuatilia kwa kina kuhusu urejeshwaji wa mikopo hiyo kwa kuwa kutorejeshwa ni miongoni mwa sababu zinazosababisha kero kwa wanaosubiri kukopeshwa na pia kukwamisha juhudi za kuwakwamua kiuchumi walengwa wa fedha hizo..

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2021

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO MWAKA YA SASA 31.03.2021 | ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.12.2020 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,649 | 3,545 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,455 | 14,184 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 19,491 | 20,280 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 33,415 | 34,926 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | 10 | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 124,502 | 132,804 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,974 | 3,670 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,176 | 2,264 |
| 16 | **Jumla ya Mali** | **204,672** | **211,673** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 23,007 | 24,256 |
| 18 | Amana za Wateja | 133,512 | 140,666 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 81 | 74 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 86 | 46 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 39 | 39 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,132 | 3,435 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **159,857** | **168,516** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **44,815** | **43,157** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 32,642 | 28,607 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,051 | 3,627 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,121 | 921 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **44,814** | **43,155** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 20,947 | 9,423 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,738 | 3,042 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,364 | 1,789 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22% | 20% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2% | 2% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80% | 82% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 61% | 63% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87% | 89% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -5% | 0% |
| (vii | Ongezeko la Mali | -3% | 1% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO YA MWAKA SASA 31.03.2021 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 31.03.2021 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.03.2021 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.03.2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,808 | 3,732 | 3,808 | 3,732 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,360 | 1,289 | 1,360 | 1,289 |
| 3 | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,448** | **2,443** | **2,448** | **2,443** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | 56 | 34 | 56 | 34 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 286 | 274 | 286 | 274 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **521** | **291** | **521** | **291** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na | | | | |
| | Miamala ya Fedha za Kigeni | 115 | 105 | 115 | 105 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 405 | 186 | 405 | 186 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 0 | - | 0 | - |
| 7 | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,210** | **1,205** | **1,210** | **1,205** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 536 | 543 | 536 | 543 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 15 | 105 | 15 | 105 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 659 | 557 | 659 | 557 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,417** | **1,221** | **1,417** | **1,221** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 366 | 201 | 366 | 201 |
| 10 | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,051** | **1,020** | **1,051** | **1,020** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,051** | **1,020** | **1,051** | **1,020** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **50** | **48** | **50** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 105 | 102 | 105 | 102 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 4 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2% | 2% | 2% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9% | 10% | 9% | 10% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 41% | 44% | 41% | 44% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 6% | 6% | 6% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 31.03.2021

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | ROBO YA MWAKA YA SASA | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|---|
| | 31.03.2021 | 31.12.2020 | 31.03.2021 | 31.03.2020 |
| Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 1,417 | 1,309 | 1,417 | 1,222 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| -Hasara katika Mali | 374 | 207 | 374 | 330 |
| -Prior Period Adjustment | 609 | (38) | 609 | - |
| -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 7,959 | (8,558) | 7,959 | 10,972 |
| -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (7,154) | 719 | (7,154) | (18,091) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,506) | (64) | (1,506) | (2,217) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,314) | 3,936 | (1,314) | 1,179 |
| -Kodi Iliyolipwa | (366) | - | (366) | (201) |
| *-Mengineyo (Bainisha)* | (26) | (412) | (26) | (912) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(8)** | **(2,900)** | **(8)** | **(7,718)** |
| Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| -Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (13) | - | (9) |
| -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 789 | 580 | 789 | (2,935) |
| -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **789** | **566** | **789** | **(2,943)** |
| Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **781** | **(2,334)** | **781** | **(10,661)** |
| -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 39,466 | 41,801 | 39,466 | 45,898 |
| -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **40,248** | **39,466** | **40,248** | **35,237** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KILICHOISHIA 31.03.2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **32,235** | **672** | **-** | **249** | **43,155** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,051 | - | - | - | 1,051 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (201) | 201 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 609 | - | - | - | 609 |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **33,694** | **873** | **-** | **249** | **44,815** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 28,381 | 775 | - | 249 | 39,404 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 3,627 | - | - | - | 3,627 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 103 | (103) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Uthaminishaji wa mali zisizohamishika | | | | | | - | - |
| Mengineyo | - | - | 124 | - | - | - | 124 |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **32,235** | **672** | **-** | **249** | **43,155** |

### BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2021

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir<br>(Mkurugenzi Mtendaji) | | 19th April, 2021 |
| Deogratias Edward Ndushi<br>Mkuu wa Fedha | | 19th April, 2021 |
| Mwita Mohamed Mwita<br>(Mkaguzi wa Ndani) | | 19th April, 2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 19th April, 2021 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 19th April, 2021 |

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

## TAARIFA MAALUM YA MIAKA 57 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

**1.0 UTANGULIZI**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo imetimiza miaka 57 tangu kuasisiwa kwake tarehe 26 Aprili, 1964. Muungano huu ambao uliunganisha zilizokuwa Dola mbili huru za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, umetupatia mafanikio lukuki katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo yanaendelea kuwanufaisha wananchi wa pande mbili za Muungano kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano huu adimu na adhimu umeendelea kudumu na kimsingi umekuwa ndio nyenzo muhimu ya Utambulisho, Amani, Umoja na Mshikamano wa Taifa letu.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Sura ya 11 Ibara ya 47 (i), jukumu la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufuatilia utekelezaji wa siku hadi siku wa mambo yanayohusu Muungano yamekabidhiwa kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa masuala yote ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa mambo yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Utekelezaji wa majukumu haya ya Kikatiba na Kisheria yamekasimiwa kwa Idara ya Muungano chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ilianzishwa rasmi mwaka 1998 kwa lengo la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**3.0 MAFANIKIO**

Muungano huu umedumu kutokana na dhamira za dhati za umoja waliokuwa nao Waasisi wetu, sera makini za Serikali zote mbili za TANU na ASP na sasa CCM. Aidha, tumeshuhudia jitihada nyingi za viongozi wa awamu zote za kuhakikisha Muungano wetu unaendelea kudumu na kuimarika na kuwa Muungano wa mfano na wa kuigwa Barani Afrika na Duniani. Pia, Serikali zetu mbili zimeweka utaratibu wa kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ambayo imeendeleza utamaduni wa kukaa pamoja kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano.

Katika kipindi cha miaka 57 ya Muungano, tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kujivunia kwa kuwa na Muungano wa kipekee uliodumu kwa muda mrefu Barani Afrika. Watanzania wamejenga umoja na misingi endelevu ya udugu baina yao, ikiwa ni uthibitisho kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unaendelea kuimarika, pamoja na kuhakikisha kuwa uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar vinaenziwa. Vilevile, pande mbili za Muungano zimejenga mifumo ya kuendesha Serikali zake kwa uwazi chini ya misingi ya demokrasia na utawala bora. Misingi hiyo imeimarika kutokana na uelewa mzuri wa dhana ya uwajibikaji kwa viongozi wa ngazi zote.

Kwa kipindi cha miaka miaka mitano 2015 hadi 2019 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesimamia vizuri uchumi wetu, ambapo ulikua kwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka. Aidha, Pato ghafi la Taifa liliongezeka kutoka shilingi trilioni 94.349 mwaka 2015 hadi kufikia shilingi trilioni 139.9 mwaka 2019; Pia, Pato la Wastani la Kila Mtu liliongezeka kutoka shilingi 2,225,099 (sawa na dola za Marekani 1,022) mwaka 2016 hadi shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,126.4) mwaka 2019. Mfumuko wa bei ulidhibitiwa kutoka wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2019 na kuongezeka kwa akiba ya fedha ya kigeni kutoka Dola za Marekani bilioni 4.09 mwezi Desemba 2015 (kiasi kinachotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 5.1) hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 4.8 mwezi Desemba, 2020 (kiasi kinachotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 5.6).

Vilevile, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 8.9 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani bilioni 9.7 mwaka 2019; na pia kuvutia uwekezaji kutoka nje wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 16.2, sawa na zaidi ya shilingi trilioni 37 mwaka 2019 ukilinganisha na Dola za Marekani bilioni 13.7 mwaka 2015. Aidha, kwa Umasikini wa kipato ulipungua hadi kufikia asilimia 26.4 kwa takwimu za mwaka 2017/2018. Kwa upande wa mfumko wa bei, tunaendelea kuwa na mfumko wa bei ulio katika tarakimu moja.

Kwa upande wa Zanzibar, mafanikio yamepatika katika kusimaimia uchumi, ambapo katika kipindi cha mwaka 2011 – 2019, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.4. Kwa mwaka 2019, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7.0 na Mfumuko wa Bei umeendelea kubakia katika tarakimu moja. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Aprili, 2020 ulifikia asilimia 3.6.

Pia, tumeshuhudia kuimarika kwa miundombinu ya barabara, usafiri wa anga, usafiri wa majini na huduma za kijamii katika pande zote za Muungano. Vilevile, tumeendelea kutumia maliasili zetu vizuri zaidi kwa manufaa ya wananchi kuliko ilivyokuwa kabla ya Muungano. Mafanikio hayo yametokana na usikivu, utulivu, uzalendo, moyo wa kujituma na kujitolea na ushirikiano wa dhati wa viongozi na wananchi. Mafanikio haya, bila shaka, ndiyo yaliwezesha Tanzania kutangazwa kuingia kundi la nchi za uchumi wa kati kutoka kundi la nchi masikini mwezi Julai, 2020.

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, kumekuwa na baadhi ya changamoto ambazo kwa ujasiri mkubwa viongozi wa pande zote mbili za Muungano wanaendelea kuzipatia ufumbuzi. Juhudi hizi zilianza mara tu baada ya Muungano wetu mwaka 1964 ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa Tume na Kamati kwa ajili ya kushughulikia changamoto za Muungano. Tume na Kamati hizo ni pamoja na:- Tume ya Dr. Salmin Amour 1984 ; Tume ya Jaji Nyalali 1990 ; Tume ya Mzee Edwin Mtei 1991 ; Kamati ya Shellukindo 1992 ; Tume ya Jaji Kisanga 1999 ; na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano mwaka 2006.

**Mafanikio mbalimbali yamepatikana kutokana na utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na Tume zilizoundwa na Serikali kama ifuatavyo: -**

i. Sheria kadhaa zimetungwa au kurekebishwa kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa mambo ya Muungano. Sheria ni pamoja na:-
- Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria Na.13 ya 1995;
- Sheria ya Uhamiaji, Na. 6 ya mwaka 1995 imetungwa na sasa watanzania wanaweza kwenda sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila vikwazo;
- Sheria ya Mamlaka ya Kodi, Na. 11 ya 1995.
- Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Na. 1 ya 1995.
- Sheria ya Tume ya Pamoja na Fedha Na. 14 1996.
- Sheria ya Biashara ya Bima ya Tanzania Na.18 ya 1996.
- Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya 1996;
- Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995;
- Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya mwaka 1995; na
- Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria Na. 5 ya mwaka 2020.

ii. Tawi la Benki Kuu ya Tanzania limejengwa Zanzibar ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefungua akaunti yake Benki Kuu na inaendelea kupata huduma za kibenki ikiwepo mikopo na ushauri juu ya kukuza uchumi kwa wananchi wa Zanzibar.

iii. Muungano wetu umeiwezesha nchi kuwa shwari, salama na tulivu. Tumeweza kulinda uhuru wetu na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar dhidi ya matishio mbalimbali. Umoja wetu na mshikamano ndani ya Muungano pamoja na uwezo na weledi tulioujenga kwa vyombo vya ulinzi na usalama vya Serikali ya Muungano ndiyo siri ya mafanikio yetu;

iv. Mfumo wa vyama vya siasa umepewa nguvu na Sheria ya Vyama vya Siasa (The Political Parties Act) Sura Namba 258, inayovitaka vyama hivyo kuwa na sura ya kitaifa. Mfumo wa vyama vingi vya siasa, umeimarisha demokrasia, uhuru wa kutoa maoni na uwazi katika uendeshaji wa shughuli za umma ikiwa ni pamoja na masuala ya Muungano. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ilianzishwa mwaka 1992 ambayo ina Ofisi kuu Dodoma na Ofisi ndogo Zanzibar. Hadi sasa, vyama vya siasa 19 vimepata usajili wa kudumu.

v. Kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano: Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano. Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vimekuwa vikijadili masuala ya kisekta, kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Ushirikiano huu ni muhimu kwa kuwa unasaidia kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka na kwa ufanisi changamoto za Muungano na za kisekta zilizopo na zinazojitokeza. Tathmini inaonesha Wizara za Kisekta zinapokutana changamoto zinapungua na Muungano unazidi kuimarika.

Jumla ya vikao 194 vya ushirikiano vimefanyika katika kipindi cha 2000 - 2021. Sekta zilizokutana ni Mawasiliano na Uchukuzi, Serikali za Mitaa, Miundombinu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Nishati, Maliasili na Utalii, Viwanda, Biashara, Masoko, Utumishi, Uratibu wa Shughuli za Serikali, Katiba na Sheria, Utawala Bora, Afya, Elimu, Habari na Utamaduni, Uchumi na Fedha.

vi. Kuelimisha umma kuhusu Muungano: Ili kuwa na jamii yenye uelewa wa masuala ya Muungano na kuweza kuuenzi na kuutetea, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali kuelimisha umma kuhusu Muungano. Wananchi wamekuwa wakielimishwa kupitia vipindi vya Redio

# TANGAZO

vii. Miradi ya Maendeleo: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushirikiana katika kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi hii imewawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira za muda kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi hiyo umefanikiwa kuinua hali ya wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii wa pande zote mbili za Muungano.

**Miongoni mwa miradi na programu zilizowahi kutekelezwa pande mbili za Muungano na kukamilika ni pamoja na: -**

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF) TASAF I, TASAF II na TASAF III Awamu ya Kwanza;
- Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani (Marine and Coastal Environmental Management Programme - MACEMP);
- Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo (Agricultural Sector Development Program – ASDP);
- Agricultural Sector Development – Livestock – ASDP – L, Agricultural Sector Support Program – ASSP;
- Programu ya Changamoto za Milenia (Millenium Challenge Account Tanzania – MCA – T);
- Mradi Shirikishi wa Programu za Maendeleo ya Kilimo (Participatory Agricultural Development Program – PADEP);
- Mradi wa Udhibiti wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Programme – SWIOFISH); na
- Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (Market Infrastracture, Value Addition and Rural Finance - MIVARF)

**Miradi na programu zinazoendelea kutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar ni pamoja na:-**

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF III) Awamu ya Pili;
- Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (Expanded Rice Production Project – ERPP);
- Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani - LDCF;
- Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini nchini Tanzania (Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania - EBARR)
- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA);
- Mpango wa kupanua usikivu shirika la utangazaji Tanzania (TBC);
- Mradi wa uboreshaji wa Elimu kupitia Global Partnership for Education; na
- Mradi wa sumu kuvu.

viii. Ujenzi wa Taasisi za Muungano Zanzibar: Serikali imekamilisha ujenzi wa wa Tawi la Benki Kuu lililopo Gulioni, Zanzibar; Ofisi ya Makamu wa Rais, Uhamiaji, Makao Makuu na Ofisi za Bunge Tunguu, Zanzibar; Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa, eneo la Uwanja wa Ndege, Zanzibar; Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu, Fumba; na Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyoko Buyu. Aidha, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imefungua Ofisi Kikwajuni, TANTRADE na NIDA zimefungua Ofisi Zanzibar, Sekretarieti ya Ajira imefungua Ofisi eneo la Shangani, TAEC na COSTECH zina Ofisi za kudumu Maruhubu, Zanzibar. Pia, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; Baraza la Taifa la Mitihani la Taifa; Idara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Mamlaka ya Usafiri wa Anga; Kampuni ya Posta Tanzania; Kampuni ya Simu Tanzania; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Tume ya Uchaguzi ya Taifa; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mamlaka ya Mapato Tanzania; Tume ya Pamoja ya Fedha; Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano; na Mamlaka ya Bima Tanzania

**Lengo la kujenga na kufungua Ofisi na Taaisisi hizo ni kusogeza karibu huduma kwa wananchi wa Zanzibar.**

## 4.0 CHANGAMOTO

Muungano umepitia vipindi vyenye matukio mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyotokea ndani na nje ya nchi na ambayo kwa njia moja au nyingine, yaliathiri uendeshaji wa shughuli za Muungano. Miongoni mwa hayo ni: -

i. Kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1967;
ii. Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977;
iii. Vita dhidi ya Iddi Amini wa Uganda mwaka 1979;
iv. Kuyumba kwa uchumi wa Dunia miaka ya 80;
v. Kulegezwa kwa masharti ya biashara na kuanzishwa sera ya uchumi huria; na
vi. Kuanzishwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1992.

Changamoto nyingine ni pamoja na uwepo wa tofauti ya Sheria kwa pande mbili za Muungano, hukwamisha utekelezaji wa baadhi ya maamuzi yanayofikiwa katika kutatua changamoto za Muungano. Hata hivyo, inapotokea changamoto ya tofauti ya sheria, Serikali zetu mbili zinashirikiana katika kuzioanisha Sheria zinazokwamisha utekelezaji.

**Hatua zilizochukuliwa**

Mifumo imara iliyowekwa ya kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoukabili Muungano wetu, imewezesha pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kupiga hatua kubwa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na hivyo kupata sifa kubwa kimataifa.

Kuundwa kwa Tume na Kamati zilizopewa majukumu ya kuchunguza na kubainisha changamoto za Muungano na kutoa mapendekezo Serikalini, ni miongoni mwa juhudi kubwa zinazochukuliwa katika kutatua changamoto zinazojitokeza. Tume na Kamati hizo ni pamoja na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano iliyoundwa mwaka 2005 na kuanza vikao mwaka 2006, imekuwa ni nyenzo muhimu katika kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa mwaka 1964. Vikao vinavyojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano vimekuwa vikifanyika katika ngazi za Wataalamu, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMT chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha changamoto zote zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utatuzi wa changamoto zilizojadiliwa na kupatiwa ufumbuzi tangu mwaka 2006, Serikali zetu mbili zimeandaa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ili kuongeza kasi ya uratibu wa vikao na ufuatiliaji wa maagizo, maelekezo na maamuzi yanayotolewa katika vikao hivyo.

Utaratibu huu, ulipitishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Pamoja cha tarehe 9 Februari, 2019, unaimarisha na kurasimisha utaratibu wa vikao vya pamoja na kuweka muda kwa vikao vya kila ngazi. Utaratibu huo pia umeainisha Kamati mbili ambazo ni Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala zilizopewa jukumu la kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazohitaji utatuzi wa haraka badala ya kusubiri utaratibu wa kawaida wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Kamati hizi huwasilisha taarifa zake kwenye vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ.

Tangu mwaka 2006, vimefanyika vikao kumi (11) vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ. Vikao hivi hutanguliwa na vikao vya Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalamu wa kisekta kutoka Serikali zote mbili. Katika vikao hivyo changamoto mbalimbali hujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

**Hoja zilizopatiwa ufumbuzi ni:-**

i. Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
ii. Utekelezaji wa Merchant Shipping Act katika Jamhuri ya Muungano na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na International Maritime Organisation (IMO);
iii. Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
iv. Uwezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kukopa Ndani na Nje ya Nchi;
v. Misamaha ya Mikopo ya Fedha kutoka IMF;
vi. Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili;
vii. Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda;
viii. Kuondoa kodi katika unga wa maziwa toka Zanzibar kuja Tanzania Bara;
ix. Gharama za Kushusha Mizigo (Landing Fees);
x. Tatizo la Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na ZRB;
xi. Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba (Serikali imesaini Mkataba na Saudi Fund tarehe 19 Aprili, 2020);
xii. Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi;
xiii. Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu;
xiv. Kuzuiwa kwa bidhaa ya sukari inayozalishwa katika Kiwanda cha Mahonda Zanzibar kuingia katika soko la Tanzania Bara; na
xv. Upatikanaji wa fursa za ushiriki wa Zanzibar katika miradi ya maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa na maendeleo ya wajasiriamali.

**Hoja zilizo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi ni:-**

i. Hoja za fedha; na
ii. Biashara baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Serikali zote mbili SMT na SMZ zinaendelea kushughulikia changamoto za Muungano kadri zinavyojitokeza.

## 5.0 MAADHIMISHO

Tunapoadhimisha miaka 57 ya Muungano wetu tunaongozwa na Kauli Mbiu isemayo: ''Muungano Wetu ni Msingi Imara wa Mapinduzi ya Kiuchumi, Tudumishe Mshikamano Wetu". Hivyo ni vema, sote tuendelee kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu adimu na adhimu kwa manufaaa yetu sote.

## 6.0 HITIMISHO

Mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka 57 ya Muungano wetu yametokana na jamii yenye umoja, mshikamano na isiyo na ubaguzi wa aina yoyote. Watu wa pande zote mbili za Muungano wanaishi na wanafanya kazi zao za kujiletea maendeleo katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kubughudhiwa.

Pia, mafaniko hayo yanatokana na ushirikiano mzuri kati ya viongozi na wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Kwa muktadha huo, mafanikio hayo siyo ya kubezwa hata kidogo na yanapaswa kulindwa, kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu zote.

**Selemani Saidi Jafo (Mb.)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO NA MAZINGIRA**

# Tatizo la majitaka Mbweni lapata tiba

SERIKALI kupitia Mradi wa Kuboresha Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP), imetenga Sh. bilioni 8.4 kwa ajili ya ujenzi wa mifereji wa maji ya mvua wenye urefu wa kilomita 8.89 katika Kata ya Mbweni.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Felista Njau.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la mafuriko katika maeneo ya Mbweni Teta, Bunju Basihaya, Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni katika jimbo la Kawe.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema serikali inatambua kero ya mafuriko katika maeneo ya Mbweni Teta, Bunju Basihaya, Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni katika Jimbo la kawe

"Awamu ya pili ya mradi huu itajumuisha mifereji ya maji ya mvua katika maeneo ya Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni, serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara, madaraja na mifereji ya maji ya mvua ili kuondoa kero ya mafuriko katika meneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam ikiwamo Jimbo la Kawe,"alisema.




# Taasisi za serikali zadaiwa bil. 3.5/- ulinzi SUMA JKT

BUNGE limeelezwa kuwa kampuni ya SUMA JKT inazidai taasisi binafsi, serikali na mashirika ya umma Sh. bilioni 3.5.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka. Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni kiasi gani SUMA JKT inazidai taasisi mbalimbali nchini.

Akijibu swali hilo, Waziri Kwandikwa alisema SUMA JKT inadai kiasi hicho na kuomba wadaiwa hao walipe ili vijana waendelee kupata ajira.

Alifafanua kuwa madeni hayo awali jumla yalikuwa Sh. bilioni 12.5 lakini baada ya kufanyika uhakiki ilibainika kuwa Sh. bilioni 12.9 na kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 8.5 zimelipwa, hivyo deni lililobaki ni Sh. bilioni 3.5.

Awali, katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni gharama kiasi gani na taratibu gani hutumika ili kupata huduma za ulinzi wa SUMA JKT.

Waziri Kwandikwa akijibu swali hilo, alisema huduma ya ulinzi kutoka SUMA JKT Guard inapatikana kupitia njia kuu nne ikiwamo idara ya masoko kutembelea wadau wa huduma ili kutangaza shughuli za kampuni na mteja mwenyewe kuwasilisha barua za maombi ya kupatiwa huduma ya ulinzi.

"Kampuni imesajiliwa katika mfumo wa manunuzi (ununuizi) ya (wa) serikali ya TANEPS ambazo wadau hasa taasisi za serikali hutumia kutangaza zabuni na ushiriki katika mchakato wa zabuni shindanishi zinazotangazwa kupitia magazeti na vyombo vya habari," alisema.

Alisema gharama ya kupata huduma za ulinzi za SUMA JKT kwa mlinzi mmoja bila silaha ni Sh. 590,000 kwa mwezi ikijumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

"Silaha moja ni sh. 129,800 hivyo mlinzi akiwa na silaha gharama yake ni Sh. 719,800 kwa mwezi na mlinzi mmoja kwa maeneo ya migodini ni Sh. 944,000 pamoja na VAT kwa mwezi," alisema.

Hata hivyo, alisema kampuni hiyo ina malindo 443 ambapo kati ya hao 259 wanalinda kwenye taasisi za umma huku 184 ni watu binafsi.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akisalimiana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abadalah Ulega, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Parachichi rasmi zao la kimkakati

WIZARA ya Kilimo imesema zao la parachichi limeingizwa kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati.

Aidha, Wizara iko katika hatua za awali za mapendekezo ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mazao ya Bustani itakayokuwa na jukumu la kusimamia mazao hayo ili kuongeza tija na kukidhi mahitaji ya soko la ndani, kikanda na kimataifa.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mgaya.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua serikali ina mkakati gani wa kuliingiza zao la parachichi katika mazao ya kimkakati.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 3,279 mwaka 2015 hadi tani 9,000 mwaka 2018.

"Katika mwaka 2018 mauzo hayo yameliingizia taifa kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.5 kutokana na masoko ya nchi za Ufaransa, Uholanzi na Uingereza," alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea kukamilisha Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Mazao ya Bustani wa mwaka 2021-2030 utakaotumika kama dira ya kuwekeza katika Sekta ya Horticulture inayojumuisha parachichi.

"Mkakati huo umehusisha wadau wote muhimu kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya 'horticulture'. Katika kuhakikisha gharama za usafirishaji wa mazao ya 'horticulture' ikiwamo parachichi zinapungua, serikali itajenga Kituo cha Huduma za Biashara ya Mazao ya Kilimo kwenye eneo la ekari 20 katika ukanda maalum wa uwekezaji Kurasini, Dar es Salaam," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kituo hicho kitakuwa cha huduma kwa pamoja chenye wataalam na miundombinu ya mnyororo wa baridi wa kuhifadhi mazao kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi kwa bei nafuu tofauti na hali ilivyo sasa ambapo baadhi ya mazao hulazimika kusafirishwa kupitia Uwanja wa Ndege wa Nairobi kwa kufuata unafuu wa gharama za huduma za usafirishaji.


Alisema parachichi ni miongoni mwa mazao ya bustani ambayo yanapewa kipaumbele katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) kutokana na umuhimu wake katika kuongeza kipato na lishe kwa wakulima na jamii kwa ujumla.

"Zao hilo ni miongoni mwa mazao yanayokua kwa kasi na limeonesha mafanikio makubwa, mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 3,279 mwaka 2015 hadi tani 9,000 mwaka 2018," alisema.

Muungano kiota cha wanawake mahiri Ukurasa 12







Ukurasa 14

**Idriss Debby, aliyeuawa na waasi wa Boko Haramu**

siasa

JUMATANO APRILI 28, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Rais na Tanzania mpya inayoweka sawa upinzani

**Na Sabato Kasika**

KATIKA hotuba yake bungeni , Rais Samia Suluhu Hassan, anatoa ahadi ya kuendelea kulinda misingi ya demokrasia ya vyama vingi, uhuru wa watu pamoja na wa vyombo na habari ili kuwa na Tanzania inayoheshimu haki ya kuwa na maoni.

Akiwa bungeni, anaonyesha mwelekeo wa serikali yake ya awamu ya sita na miongoni mwa mambo anayogusia ni kuendeleza uhuru na demokrasia kwa vile vinachochea maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, lakini anataka uhuru unaozingatia mipaka.

Anatangaza azma ya kukutana na viongozi wa vyama vya siasa ili kwa pamoja waweke mwelekeo wa kuendesha siasa zenye tija.

Kujua zaidi nia hiyo, Nipashe inazungumza na wachambuzi wa siasa kupata maoni yao kuhusu hatua na ahadi hiyo ya Ikulu.

Said Msonga ni mchambuzi wa siasa ambaye anasema, Rais inaonyesha jinsi alivyodhamiria kufungua ukurasa mpya, na kwamba hiyo ni fursa muhimu kwa viongozi wa vyama vya siasa.

"Ni lazima kuwe na mawazo mbadala, kwani siasa za ushindani wa hoja ni za muhimu katika ujenzi wa taifa, zinapofanyiwa kazi, zinaleta manufaa kwa nchi hivyo hatua aliyoahidi kuchukua ina afya kwenye demokrasia," anasema Msonga.

Anaeleza kuwa siasa za ushindani wa hoja na kuheshimiana zinaleta tija kwa wananchi, na kwamba ndizo ambazo wengi wanatamani ziendelezwe.

"Ushauri wangu kwa viongozi wa siasa ni kuwa hiyo ni fursa ya pekee kwao ambayo itakuwa imefungua ukurasa mpya baada ya miaka mitano ya malalamiko ya kuzuiwa kufanya siasa," anasema.



Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia bungeni wiki iliyopita.. **PICHA: MTANDAO**

Mchambuzi huyo anawataka viongozi wa vyama vya siasa na hasa upinzani, kujenga hoja na kuishauri serikali kwa lugha ya staha ili hoja za muhimu iweze kuzichukua na kuzifanyia kazi.

Mchambuzi Abdulkarim Atiki, anasema, Rais anaeleza mwelekeo wa serikali yake, ambao ni kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, kuendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya.

"Miongoni mwa mengine mapya ni kukutana na viongozi hao, kujadili hali ya kisiasa nchini na huenda wakajadili kilio cha muda mrefu cha viongozi cha kutaka waruhusiwe kuendesha shughuli za kisiasa," anasema Atiki.

Kadhalika anasema, ikiwa ni hotuba yake ya kwanza bungeni tangu alipoapishwa kuliongoza taifa, kufuatia kifo cha mtangulizi wake John Magufuli, imeweka wazi mwelekeo wa serikali yake.

"Rais kutamka kuwa anakusudia kukutana na viongozi wa vyama vya siasa kwa ajili ya uboreshaji wa demokrasia na uhuru katika nchi yake ni jambo la kungwa mkono," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hellen Kijo-Bisimba, anasema, hatua ya Rais kutoa ahadi ya kukutana na viongozi wa vyama vya siasa ni pambazuko jema.

"Ninasema ni dalili njema, kwa sababu wahusika watapata nafasi ya kuwasilisha maoni, dukuduku na kero za muda mrefu ambazo wamekumbana nazo kwa miaka mitano iliyopita," anasema Kijo-Bisimba.

Anasema, tangu mwaka 2016, vyombo vya dola vilivizuia kinyume na katiba na sheria shughuli za siasa za vyama vya upinzani hadi uchaguzi mkuu wa mwaka jana, hali ambayo anadai ni kero.

"Hilo na mengine mengi, ninaamini yanaweza kuwa miongoni mwa ajenda ambazo viongozi wa vyama hivyo watayafikisha kwa Rais ambaye kwa kweli ameonyesha nia ya kuleta mabadiliko katika siasa za Tanzania," anasema.

Mwanaharakati huyo wa haki za binadamu anasema, kwa miaka mitano hakukuwa na siasa za ushindani hali ambayo anaamini imesababisha uhai wa vyama vya siasa kuwa mashakani kutokana na kuzuiwa kujijenga.

"Wanasiasa wamepata ruhusa ya kukutana na Rais Samia, hivyo niwaombe wajipange vizuri ili wawasilishe hoja zenye mashiko kwa Rais, hatimaye waruhusiwe kuendesha siasa za ushindani kwa manufaa ya taifa," anasema.

Anaongeza kuwa kila unapomalizika uchaguzi, huwa ni mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi mwingine, na kwamba, baada ya uchaguzi mwa mwaka 2015, vyama vilizuiwa kuendelea na maandalizi ya uchaguzi mwaka 2020.

"Kulikuwa na hoja kwamba, Watanzania wanataka maendeleo, hivyo vyama viache siasa vifanye maendeleo. Lakini ukweli ni kwamba kufanya siasa ni sehemu ya maendeleo ya nchi," anasema.

Anafafanua kuwa siasa ni maisha ya kila siku, haina muda, na kwamba inawezekana Rais ameliona hilo na sasa anataka aweke mambo sawa ili wanasiasa wawe uhuru kuendesha siasa zenye tija katika nchi yao.

"Vyama vya upinzani vipo, lakini kilichokuwa kikifanyika ni kama nchi hii ni ya chama kimoja, hali iliyosababisha manung'uniko kutoka kwa wadau wa siasa kila kona ya nchi," anasema.

Anasema, anaamini viongozi wa vyama vya siasa watakuwa na hoja nyingi za kumweleza Rais kwa manufaa ya nchi, iwapo watakuwa wamezipangilia kwa busara na hekima bila kuwa na jazba.

"Kwa mfano uchaguzi wa serikali za mitaa na hata uchaguzi mkuu wa mwaka jana, kuna mengi ya kuzungumzia ambayo kwa namna moja au nyingine umeacha sintofahamu kwa vyama vya upinzani nchini," anasema mwasisi na mkurugenzi wa zamani wa LHRC.

Kijo-Bisimba anasema, huu ni wakati wa vyama vya siasa na wanasiasa kuacha tofauti zao na kukutana na serikali kujadili hali halisi ya kisiasa nchini na hatimaye kuwa na mikakati ya kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini.

# Muungano kiota cha wanawake mahiri

## •Ni Rais Samia, mawaziri wizara nyeti



Waasisi wa Muungano, Julius Nyerere (kulia ) na Sheikh Abeid Amani Karume, ni waanzilishi wa chachu ya maendeleo ya wanawake kisiasa .



**Na Gaudensia Mngumi**

HONGERA Watanzania Bara na Wazanzibari kwa kukata keki na kusherehekea miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mwaka huu maadhimisho yanaongozwa na Amiri Jeshi, Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye ni tunda la Muungano ambao kwa takribani miongo sita umekuwa na mafanikio makubwa katika kuwaibua na kuwafikisha wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi.

Nipashe inazungumza na Jane Magigita, Mkurugenzi wa Taasisi ya 'Equality for Growth', anayesema Muungano umekuwa mhimili wa kuwafikisha kinamama kwenye nyadhifa za juu na ukiendeleza usawa kijinsia:

**SWALI: Unazungumziaje masuala ya wanawake na Muungano?**

**JIBU:** Muungano umewezesha kupatikana wabunge na wawakilishi ambao wanaingia kwenye vyombo vya kutunga sheria, yaani Bunge na Baraza la Wawakilishi. Zanzibar ikiwa na wabunge pamoja na wawakilishi ambao wanaongeza idadi ya wanawake kwenye mihimili hiyo miwili ya dola.

Niseme kuwa Muungano umetambua umuhimu mkubwa wa wanawake katika uchumi wa Zanzibar na Tanzania na kwamba mafanikio yaliyopo sasa kuna mchango mkubwa wa wanawake.

Kuna wanawake wanaozalisha kwenye kilimo, viwanda, wanaofanyabiashara ndogo ndogo, wapo wanaotoa huduma na uchumi ulivyo leo kutokana na kazi nyingi na muhimu zinazofanywa na kinamama.

"Tusisahau malezi, wanawake wana mchango mkubwa wa kulea watoto ambao ndiyo viongozi unaowaona leo, ni zao la kazi za mwanamke ndani ya familia hivyo, huwezi kuacha jukumu lao, wanahusika sana na ulezi, ulinzi na makuzi."

**SWALI: Kwa miaka 57 ya Muungano unaona imeacha alama gani kwa wanawake?**

**JIBU:** Umekuwa ni ngazi ya wanawake kupandia hadi kufikia nafasi za juu za uongozi. Kwa mfano Rais Samia ni zao la Muungano. Amekuwa mwakilishi na hatua kwa hatua amekuwa Waziri akiongoza wizara mbalimbali Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ya Muungano hadi kufikia hatua ya kuwa Rais wa Jamhuri.

Pia Muungano umewatoa mawaziri walioongoza wizara nyeti hasa Wizara ya Fedha na ya Mambo ya Nje.

Wizara hizi nyeti ziliongozwa na kinamama majasiri kama Amina Salim Ali,yupo Zakia Meghji, aliyeongoza Wizara ya Fedha awamu ya tatu pamoja na Saada Salum Mkuya, ambaye naye ameongoza ofisi hiyo.

Kinamama hao wameongoza wizara hizo nyeti na Amina Salum Ali, amechomoza zaidi na kuwa mgombea urais aliyefikia nafasi za juu kuwa miongoni mwa tatu bora ya wagombea urais mwaka 2015.

Muungano umechangia kwenye kuibua viongozi hao ambao ni mafanikio makubwa kwa wanawake wa Tanzania.

> Niseme kuwa Muungano umetambua umuhimu mkubwa wa wanawake katika uchumi wa Zanzibar na Tanzania na kwamba mafanikio yaliyopo sasa kuna mchango mkubwa wa wanawake

**SWALI: Unadhani wanawake wanataka Muungano wa namna gani leo?**

**JIBU:** Kinamama wanataka Muungano unaojibu maswali ya namna bora ya kuondoa changamoto za unyanyasaji kinamama, watoto, udhalilishaji, ubakaji, mimba za watoto na kutelekeza familia kwa visingizio mbalimbali.

Wanawake wanataka kuona masuala nyeti, magumu na yanayowakwamisha kwenye kufikia malengo yao kielimu, kiafya, kisiasa, kiuchumi na kwenye usalama wao na watoto yakijibiwa kwa kupata utatuzi wa kudumu.

Tunapenda kuona amani ikiendelea kwani Muungano umeongeza maingiliano na fursa miongoni mwa Watanzania. Kwa mfano, utaona watu kutoka Pemba na Unguja wamepata makazi ya kudumu na wanafanyabiashara zao Bara.

Tunaona kuna ushirikiano na ukaribu na udugu huo unaendelea na Watanzania waendelee kuwa na amani na usalama ambao ni muhimu kwa kinamama na familia.

**SWALI: Una ujumbe gani kwa wanawake wakati huu Rais Samia anapoliongoza taifa kuadhimisha miaka 57 ya Muungano?**

**JIBU:** Kuwapo kiongozi mwanamama kunamaanisha kuwa anatazama na ataangalia mambo kwa jicho tofauti na la kipekee.

Tanzania ina Rais anayefahamu changamoto za wanawake, watoto, familia, vijana na anazo hisia kuhusu mambo anayoyazungumzia ili kuboresha maisha yao.

Anajua hali ilivyo kwenye familia na anapozungumza anafahamu changamoto zinazowakabili wanawake, wanaume, watoto, wazee, wasiojiweza na wahitaji ndani ya taifa hili.

Tunaamini atakuwa na jicho tofauti katika kuchambua na kuweka mikakati ya ulinzi wa watoto kukabiliana na mimba za utotoni na kudumisha haki za watoto na makundi maalumu.

**SWALI: Ninini wanawake wa Tanzania na Zanzibar wategemee kutoka kwenye awamu hii?**

**JIBU:** Ninaamini wanategemea kuona mabadiliko chanya kwenye elimu, afya, kilimo, biashara ndogo ndogo, umiliki wa ardhi, haki mbele ya sheria na urahisi katika kazi zao kwa vile maeneo hayo ndiyo yanayowabeba wanawake wengi wa Zanzibar na Bara.

Hivyo, hata maisha ya wanawake vijiji yanatarajiwa kubadilika kwa kuwa jicho la Rais litaangalia na kuchambua pamoja na kuelekeza namna tofauti na bora ya kushughulikia masuala hayo ambayo yamekuwa changamoto miaka 60 ya Uhuru sasa na leo 57 ya Muungano.

**SWALI: Kwa vijana na mabinti wanaoishi Zanzibar na Tanzania Bara wanaona nini katika uongozi wa serikali ya awamu ya sita?**

**JIBU:** Vijana hasa wanawake popote walipo, wawe shuleni, vyuoni, kazini wajitie moyo na kujiaminisha kuwa kila kitu kinawezeka kwa kuona kuwa Rais anaweza watumie falsafa yake kufanikisha kile wanachofanya hasa mabinti na wanawake.

Kwa ujumla ni wakati wa Watanzania kufahamu kuwa taifa linahitaji kuwa na usawa kijinsia. Kuondoa fikra kuwa mwanaume ndiye kiongozi na mwanamke ni mfuasi wake. Aidha kuachana na mitazamo kuwa mwanaume ana nguvu na mwanamke ni dhaifu.

Ndiyo maana Rais anakumbusha kuwa Mungu hakuweka ubongo dhaifu kwa mwanamke, kila mmoja amekamilika na ameumbwa kwa utimilifu.

UCHAMBUZI

# Kwa jitihada hizi, Rais atawainua kinamama

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Samia katika moja ya ziara za kutembelea wagonjwa hospitalini kuendeleza jitihada za kuboresha huduma za afya. **PICHA: MTANDAO**

WANAWAKE ni zaidi ya asilimia 50 ya raia wa nchi hii, lakini licha ya wingi wao ni waathirika wakubwa wa umaskini na madhila mengine mabaya kama afya duni na vifo vya uzazi.

Na kama haitoshi, wengi zaidi hawajui kusoma na kuandika, ndiyo idadi kubwa ya wasio na ajira tena ni waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia. Lakini katika upungufu huo ni wazalishaji wakubwa mashambani, watunza familia na wabeba majukumu mengi yanayohusu maendeleo ya taifa.

Kwa hiyo, wanabaki kuwa mhimili wa maendeleo ya taifa, kwa sababu hiyo lolote linalofanyika Bara na Zanzibar haliwezi kukwepa juhudi za kufikia ustawi wa wanawake walio nguzo ya Tanzania.

Hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa bungeni hivi karibuni, haijawasahau kinamama, imesheheni masuala ya kuwahakikisha ustawi wanawake na watoto kwa kutambua kuwa ndiyo uti wa mgongo wa taifa.

Baadhi ya masuala muhimu yanayogusa moja kwa moja na yanayomlenga mwanamke ni pamoja na:

Afya, Rais Samia, anaahidi kujenga hospitali, vituo vya afya na kuongeza idadi ya watu wanaotumia bima ya afya na pia kuboresha huduma za utaalamu wa kibingwa na kuzifikisha kwenye hospitali za rufani. Amebainisha nia ya kuboresha maisha ya mwanamke.

Endapo yote hayo yatafanikiwa ni ulinzi kwa wajawazito na wazazi, ni uhakika wa tiba ya wanawake maskini na watoto wao ambao wanastahili kunufaika na bima ya afya.

Matamanio hayo ya serikali ni habari njema kwa kinamama ambao wana uhakika watoto wao, wahitaji na wazee wanaowatunza majumbani watatibiwa na kuwa na maisha na afya bora.

Kusikitishwa na vifo vya wanawake, anapoeleza hadharani kuwa binafsi anasikitika mno na kuumizwa na vifo vya wanawake, wajawazito na watoto vinavyotokana na uzazi na magonjwa mengine ambavyo vingeweza kuzuiliwa ni uelekeo kuwa tatizo hilo linapata ufumbuzi kwa kuimarisha huduma za afya.

Rais anaposema hayo anaamini kuwa hata apolikuwa anazungumza Dodoma kuna wanawake wanaojifungua wodini, wapo wanaokata roho wakati huo kutokana na kukosa huduma ya kutibu matatizo ambayo yangezuilika. Pia anazo hisia kuwa kuna kinamama Zanzibar na Bara wanaohuzunika kwa sababu watoto wao wamekufa kutokana na lishe duni, kukosa tiba na huduma bora za jamii.

Kilimo, Rais anapolihutubia bunge anaahidi kuboresha kilimo kwa kuongeza uzalishaji kihekari, kujenga skimu za umwagiliaji na kuongeza uzalishaji wa mifugo ya kisasa ili kupata nyama na maziwa zaidi.

Ahadi hiyo inawagusa wanawake walio washirika wakuu wa kilimo na endapo serikali inakiimarisha, itaboresha afya za watoto kwa kupunguza utapiamlo na udumavu, lishe duni na ukosefu wa vyakula shuleni.

Rushwa, anaahidi kuitokomeza na kutaka mahakama zihukumu kwa haki hili ni suala analolisema akifahamu kuwa wapo wanawake wajane wanaokataliwa haki mahakamani kisa hawana cha kuwahonga (rushwa) wazee wa baraza la ardhi, mahakimu na hata polisi polisi licha ya kwamba wameporwa mali zao baada ya kufiwa na wenza au kudhulumiwa.

Usawa kijinsia na kuteua wanawake wengi zaidi ni eneo analoligusia. Rais, anafahamu kuwa mfumo dume umewaondoa wanawake kwenye uongozi na umekuwa tatizo kubwa linalowakwamisha kwenye maendeleo.

Anataka kurekebisha hali hiyo kuondoa unyanyasaji wa kingono vyuo vikuu, kuepusha wahadhiri kuwatumia mabinti vibaya kingono na wanapokataa wanawafelisha.

Ndiyo maana kwa uelekeo huo inaonyesha kunahitajika uteuzi wa wakuu wa vyuo , wakuu taaluma na maofisa wengi wanawake vyuoni ili kukomesha mazoea kama hayo.

> Katika uelekeo huo Rais, anataka Tanzania liwe taifa linaloheshimu haki za binadamu, lenye usawa na haki bila kujali jinsi za watu. Anatamani kuona watoto wote wanasoma, wanaajiriwa na kufanyakazi zenye staha ama wanajiajiri na kumudu maisha yao.

Anafahamu watoto wa kike hawaendi shule kisa tu wamezaliwa wanawake, kaka zao ndiyo wanaosomeshwa lakini mabinti wanaozwa, yote hayo ni kuendeleza unyanyasaji kijinsia.

Lakini, kwa uteuzi wa wanawake wengi viongozi kuna uhakika kuwa watafuatilia masuala ya elimu, ustawi wa wasichana na kukomesha mila na mazoea maovu yanayowarudisha nyuma wasichana.

Uteuzi wa kinamama viongozi utazimulika kata, vijiji na wilaya na kaya ili kuukabili unyanyasaji huo.

Katika uelekeo huo Rais, anataka Tanzania liwe taifa linaloheshimu haki za binadamu, lenye usawa na haki bila kujali jinsi za watu. Anatamani kuona watoto wote wanasoma, wanaajiriwa na kufanyakazi zenye staha ama wanajiajiri na kumudu maisha yao.

Anataka wanawake waelimike, wasiwe wahanga wa umaskini, unyanyasaji wa kijinsia na wanyonge. Aidha, hotuba yake inaashiria kuwa anapenda kuwe na haki na maisha bora kwa wote ili taifa listawi, kuendelea na kufikia maendeleo endelevu huku Tanzania ikibakia kuwa nchi ya amani na utulivu.

Anafahamu kuna unyanyasaji dhidi ya wanawake umeota mizizi kwa vile wapo wanaoteswa na kudhulumiwa na wenzi, marafiki kuna wanaokosa haki mahakamani, mitaani hata wakiingia benki wananyimwa mikopo kisa unyonge na kukosa mtu wa kuzungumzia, kufuatilia na kutatua shida zao.

Ndiyo maana analitafutia dawa kwa kuteua wanawake wengi watakaosaidia kufanikisha maendeleo na usawa wa kijinsia.

Maji, Rais Samia, anaahidi bungeni kusafisha mamlaka za maji na kuweka wahandisi maji makini na weledi mikoani pamoja na kuchimba maji ya mvua sehemu kame.

Suala hilo limewagusu wanawake wengi kwa vile ni waathirika wa tatizo la maji ambalo limesababisha hata kutelekezwa na wenza.

Hotuba yake inaonyesha kuwa anatamani waondokane na kero ya kuamka alfajiri au kukesha visimani kusakama maji.

Aidha, analenga kuepusha vifo kwani wapo waliouawa na wanyamapori vichakani wakisaka maji. Pia, kukosa maji kumesababisha malalamiko hospitalini na shuleni kwa vile ni sababu maji yanatajwa kuwa ni chanzo cha mimba kwa wanafunzi shuleni na mitaani.

Kwa kutekeleza azma hiyo wanawake wa Tanzania wanaweza kuishi na kupunguza mzigo mzito wa changamoto lukuki zinazowakabili.

## IDRISS DEBY

# Mbabe aliyezimwa na risasi za Boko Haram

## •Ni zao lililomwangusha Hussein Habre

**Na Ani Jozeni**

KIFO cha aliyekuwa Rais wa Chad, Idriss Deby, kimezua taharuki barani Afrika , huku wengi wakikataa kuamini taarifa kuwa alifia vitani kaskazini ya nchi hiyo kama ilivyotangazwa.

Hata hivyo baadhi ya wachunguzi wa habari wanaanza kuamini maelezo hayo kwa sababu mbili, kuwa wa kwanza kufaidika na kifo hicho ni mwanae, Jenerali Mamahat Deby Itno (37), ambaye mara moja aliapishwa kuwa rais wa kipindi cha mpito hadi uchaguzi mkuu miezi 18 kuanzia sasa. Endapo ni kundi katika jeshi ambalo limeandaa mpango wa kumdhuru amiri jeshi wao, ingekuwaje wamwandae mwanae kumrithi?

Ukisoma visa vya jinsi vita kaskazini mwa nchi hiyo inavyoendeshwa, unagundua kuwa waasi wamekuwa na uwezo wa kujongea ndani kutoka kaskazini hadi katikati ya nchi hiyo, na hata kuanza kuelekea kusini.

Rais Deby mwenyewe anatokea kaskazini mashariki ya Chad, licha ya kuwa mji mkuu wa Ndjamena uko katikati kuelekea zaidi kusini.


Deby akimwondoa madarakani kivita Hissein Habre, ambaye wakati huo alikuwa akiungwa mkono na Ufaransa, kipindi waasi wa kaskazini (na nyakati tofauti wakiwa ndiyo watawala kabla ya kuondolewa kijeshi na 'waasi' wengine) zama hizo wakiungwa mkono na Libya.

Vita nchini Chad, kama ilivyo Sudan, Ethiopia, Somalia au ukanda wa magharibi wa Afrika hasa ule wa eneo la nusu jangwa la Sahel, ni utamaduni katika sehemu hiyo. Jiografia ya siasa katika Afrika ina vielelezo kuwa nchi ambazo watu wake zaidi ni wakulima wanakuwa na mwelekeo wa amani hata kama wana upungufu ya kina kwingineko katika utamaduni, mataifa yenye makabila makubwa ya wafugaji ni tofauti, kwani wakati mkulima analazimika kubaki anakoishi kwa jadi na kuwe na amani ya kuendeleza kilimo, mfugaji wa Afrika anakaa popote.


Kadhalika anakaa mjini na wafuasi wake watapigana kokote, wanahamia au kukaa kwa muda wowote mahali popote. Ndiyo mazingira ya vita vya 'waasi' isiyomalizika.

Kama ilivyo kwa watawala wengine wa kijeshi waliofia vitani au ikulu, mfano Zaire au Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo mwaka 2001, aliuawa Rais Joseph Desire Kabila na wapinzani walio karibu naye kulilazimisha mawane Joseph Kabila kuchukua madaraka.

Sababu zinaweza kuwa rahisi kuwa mwanao ni mtu unayemwamini na katka mazingira ya vita, inakuwa muhimu ajengewe ushujaa na ukakamavu awekwe juu ya vikosi muhimu vya jeshi. Ni utawala halisi wa kifalme kwani ndugu yako mkishirikiana madaraka anaweza kukudhuru (kama mizozo inayotokea falme za Kiarabu) lakini mwanao hawezi.



Hissein Habre, kiongozi wa waasi aliyeenguliwa na Debby. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Idriss Debby, aliyeuawa na waasi wa Boko Haramu.

Licha ya kuwa nchi za Afrika hazina utawala wa kifalme katika hali halisi, mazingira yanachochea kuwa na mifumo ya utawala wa kifalme au ukoo ni aina ya mamluki, ambako makundi ya wapiganaji wenye utii binafsi kwa mkuu wa nchi, yaani mwajiri wao, wanakuwa na nguvu.

Hali hiyo inajitokeza kwa kukosekana uwiano kati ya nguvu za raia na nguvu za serikali, kwani raia wanakuwa hawana umoja wenye dhamira ya kumtii kiongozi aliyeko madarakani, na pia hawana uwezo wa kuunda mfungamano wowote, uwe wa kiraia au wa kijeshi, wa kuiondoa serikali iliyoko madarakani.

Kelele za wanaowapinga zinasikika zaidi katika hali hiyo, lakini uchaguzi unapofika mamilioni hupiga kura kumchagua aliyeko madarakani, kwa sababu rahisi ya kutaka amani. Kwa sehemu isiyo ndogo hayo pia yalikuwa ndiyo mazingira ya uongozi wa Idris Deby, kuanzia mwaka 1990 alipotwaa madaraka ya kijeshi hadi wiki iliyopita akiuawa kwenye medani za vita.

Taarifa zinaonyesha kuwa Ufaransa itajilaumu kwa mkasa huo kwa sababu wana kombania angalau moja inayosaidia jeshi la Chad siyo moja kwa moja kupigana na waasi ila kutoa taarifa za mizunguko ya vikundi vya wapiganaji waasi.

Hata hivyo tatizo kubwa zaidi halikuwa ni kutokuwapo kuungwa mkono kikamilifu na Ufaransa ila migawanyiko ndani ya jeshi la Chad, ambalo limegawanyika kwa makundi ya kikabila, kikoo na utii kwa viongozi binafsi wanaoshiriki biashara mbalimbali.

Kuwapo kwa mazingira ya uasi nchi kadhaa ni kuwezesha kuzuka kwa 'soko holela' la madini, kuyachimba chini ya mtutu wa bunduki na kumuuzia Mzungu au Myahudi kama ilivyo kwa Congo DRC, ambako wageni wanangoja madini yavunwe. Katika biashara hiyo isiyokuwa na udhibiti, wala kutozwa kodi au usimamizi hawataki kusikia suala la amani.

Kama zilivyokuwa nchi nyingine zenye watawala wa muda mrefu wa kijeshi, Rais Deby pia 'alikanyaga matope' ya demokrasia ya vyama vingi, lakini madaraka kamili yalibaki mikononi mwake.

Kifo chake hakishangazi wachunguzi wa habari kwani ni mnufaika alifaidika na sera ya Kanali Gaddafi ya kusaidia makundi ya waasi wanaotambua ushawishi wa Libya na yeye mwenyewe kama'Mangi Mkuu wa Afrika' mwingine akiwa ni Jenerali Museveni huko Uganda, kupata silaha, fedha na hata wapiganaji kuondoa serikali iliyokuwa madarakani.

Si jambo la ajabu kama wapiganaji wanatokea Libya bila kutazamiwa, ikidhaniwa pametulia na hivyo amirijeshi anaweza kutembelea huko kuwasalimu askari kabla ya kuapishwa.

Bado wachambuzi wa siasa za Chad hawajafikia tamati hii au ile kama kutakuwa kweli na kipindi cha mpito halafu ufanyike uchaguzi huru na wa haki nchini humo, moja ya matazamio ikiwa ni hisia kuwa upinzani unaweza kutwaa madaraka ulete mabadiliko.

Wenye ufahamu wa siasa za Afrika haielekei kuwa watakimbilia ndoto hizo, kwani itategemea uwezo wa Jenerali Itno Mahamat Deby, kutwaa usukani wa uongozi na kufaulu, kama ilivyokuwa kwa Joseph Kabila hapo DRC.

Na siyo ajabu pia akawa na mazingira mazuri ya kukusanya kura za kutosha ukifanyika uchaguzi wakati huo, kama 'akipanga kete zake vizuri,' yaani akionyesha kujali watu wa maeneo tofauti, waridhike naye ili amani iendelee, si katika nchi yote ila eneo ambalo jeshi analoliongoza linasimamia. Inavyoelekea kuna safari ndefu hadi kufikia demokrasia nchini Chad.







Baadhi ya wabunge wakiingia bungeni, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuendelea na vikao vya Bajeti. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri aridhishwa utendaji REA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema serikali imeridhishwa na utendaji kazi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na wizara imekuwa ikijivunia kazi zinazofanywa katika usambazaji wa umeme vijijini.

Dk. Kalemani aliyasema hayo juzi jijini Dodoma wakati akifunga kikao kazi cha siku mbili cha kutathimini utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini kilicho washirikisha REA na TANESCO.

Alisema kazi kubwa inayofanywa hivi sasa na wakala huo ni ya kujivunia kutokana na kasi waliyonayo kufikia azma ya serikali kuvifikia vijiji vyote mwishoni mwa mwakani.

Aidha, aliwataka REA kuhakikisha wanaongeza kasi ya usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini ili kufikia malengo ya serikali kwa vijiji vyote kuwa na nishati hiyo ifikapo Desemba 2022.

"Azma ya serikali ni huduma hii ya umeme hifikia vijiji vyote nchini ifikapo Desemba 2022, hivyo kuanzia sasa tuna miezi 18 kukamilisha zoezi (kazi) hili (hii) ili kuvifikia vijiji vyote vilivyobaki" alisema.

Pia Dk. Kalemani aliitaka REA kulinda hadhi yake kwa kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali ambayo hayajafikishiwa huduma ya nishati ya umeme.

"Ndugu zangu mafanikio ya nchi hii yanategemea nishati ya umeme ambayo ni kazi yenu ninyi REA na TANESCO. Vigezo vilivyofanya tuingie kwenye uchumi wa kati ni umeme umechangia kwa kiasi kikubwa sana," alisema Dk. Kalemani.

Pia alisema serikali imeweka malengo na mipango yake kuhakikisha wananchi kila kijiji wanapata nishati ya umeme hivyo REA, wahakikishe vijiji vyote vinapata huduma hiyo muhimu.

"Maeneo ambayo REA imekuwa na mafanikio ni kufikisha umeme katika vijiji 10,300 sawa na asilimia 87 kati ya vijiji 12,268 nchini na lengo letu ni kuhakikisha vijiji vyote vinapata nishati ya umeme," alisisitiza.

Naye Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, aliipongeza REA kwa kufanya kazi nzuri ya usambazaji umeme nchini na kuitaka kuendelea kuongeza juhudi.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Advera Mwijage, alisema watahakikisha maagizo yote yaliyotolewa na waziri wanayafanyia kazi ili wananchi wote wanufaike na nishati hiyo.

# Wataka fedha mfuko korosho kurudiwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa korosho nchini wameiomba serikali kurudisha fedha zilizokuwa kwenye mfuko wa korosho ambazo zilihamishiwa mfuko mkuu wa serikali ili kuongeza tija katika uzalishaji wa zao hilo.

Aidha, mwaka 2018 Bunge lilifanyia mabadiliko ya sheria iliyoondoa mgawo wa ushuru wa kuuza korosho nje ya nchi kwenda nje ya mfumo wa zao hilo.

Kabla ya sheria hiyo kupitishwa, fedha za ushuru zilikuwa zikitumika kuwasaidia wakulima kupata pembejeo na viuatilifu kwa asilimia 100, lakini baada ya sheria hiyo wakulima walianza kujinunulia hali ambayo inaelezwa imesababisha kupungua kwa uzalishaji.

Wadau hao walitoa ombi hilo jijini Dodoma juzi wakati wakichangia katika kikao cha tathmini ya uzalishaji na masoko ya korosho msimu wa mwaka 2020/21 na maandalizi ya msimu wa mwaka 2021/22.

Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, alisema ili kupunguza mzigo kwa wakulima na kuongeza tija katika zao hilo, fedha iliyokuwa inakusanywa kutokana na ushuru na kwenda kwenye mfuko mkuu inatakiwa kurudi ili kusaidia korosho.

Nnauye alisema Wizara ya Kilimo kwenye bajeti yoo wanatakiwa kuja na mapendekezo kuwa baadhi ya fedha hiyo itapelekwa kwenye korosho kulingana na sheria inavyoeleza.

"Kama lengo la kuipeleka fedha hiyo mfuko mkuu ilikuwa ni kwa ajili ya kuzisimamia vizuri katika zao hilo, kwa nini mzigo uliokuwa unabebwa na fedha hizo abebeshwe mkulima kinyume cha sheria," alisema.

"Tuangalie namna nzuri ya kuwasaidia wakulima vinginevyo tutakuwa tumepora fedha na kupeleka kwenye matumizi mengine wakati huo tunataka kukamua kutoka kwenye korosho.

"Na uzuri namba hazidanganyi tulipofanya vizuri namba ya uzalishaji ilikuwa juu na tulipolikoroga ikashuka," aliongeza.

Mbunge wa Viti Maalumu, Riziki Lulida, alisema kuna haja ya kufanyia mabadiliko sheria hiyo ili fedha hizo zirudi kusaidia zao la korosho kwa kuwa kwa sasa wakulima hawapati pembejeo na viuatilifu kwa wakati.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa kilimo (TARI) Naliendele, Dk. Fortnatus Kapinga. alisema takwimu zinaonyesha kuwa miaka miwili mfululizo uzalishaji wa korosho nchini umepungua ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2017/18 ambapo uzalishaji ulifikia tani 313,826.

Dk. Kapinga alisema msimu wa mwaka 2019/20 uzalishaji ulikuwa tani 232,682 na mwaka 2020/21 uzalishaji ulikuwa tani 206,719.

Pia alisema Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI, ilifanya utafiti mwaka jana ili kujua sababu za kupungua kwa uzalishaji na kubaini sababu mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa elimu ya kutosha kwa wakulima.

Alisema asilimia 68.3 ya wakulima waliohojiwa walitumia mchanganyiko wa viuatilifu uliokuwa chini ya kiwango huku asilimia 24.70 ya wakulima walichanganya zaidi ya kiwango kinachotakiwa.

Hata hivyo, alisema asilimia saba ya waliohojiwa walibuni namna ya kupulizia mikorosho mingi shambani kwa kutumia dawa kidogo.

"Mfano badala ya mkulima kuchanganya milimita 2.5 za viuadudu kwenye lita moja ya maji pia Sulphur ya unga, alichanganywa na maji na kiuadudu na kiuadudu ilichanganywa na Sulphur ya unga na kuanikwa juani kisha kupuliziwa kwenye mikorosho," alisema

# DC ataka umakini mpango wa TASAF

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, ametaka kuwapo kwa umakini na uadilifu ili kufikia malengo ya serikali wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF).

Nyamoga alisema hayo juzi wakati kifungua kikao kazi cha kujenga uelewa kwa wadau kuhusu sehemu ya pili ya awamu ya tatu ya TASAF.

Alisema halmashauri hiyo imejizatiti kuhakikisha malengo ya mpango huo yanafikiwa sambamba na kuhakikisha wote walioainishwa na kuandikishwa kwenye mpango wananufaika.

"Ili malengo hayo yafikiwe kwa ukamilifu ushiriki wa wadau wote katika ngazi mbalimbali unahitajika sana, muundo wa sehemu ya pili ya mpango umezingatia sana changamoto ambazo zilijitokeza katika utekelezaji wa awamu ya kwanza" alisema Nyamoga.

Alisema usimamizi na ufuatiliaji umeimarishwa katika ngazi ya mkoa , halmashauri na kata kwa kuhusisha watumishi zaidi kufuatilia shughuli za mfuko, utekelezaji utaimarisha uwazi, uwakibikaji na kutoa fursa kwa makundi mbalimbali kushiriki kwa kutumia mfumo madhubuti wa kubaini walengwa katika vijiji, mitaa na shehia.

"Tukafanye kazi kwa uadilifu ili tufikie malengo ya serikali kupitia kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya Tasaf ya kupunguza umaskini na kuchochea ukuaji wa uchumi ukiwamo ule wa viwanda ambavyo ni agenda muhimu ya serikali," alisema.

Katika hotuba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, iliyosomwa na Mtaalam wa Utafifi wa TASAF, Tumpe Lukongo, alisema tathimini ya utekelezaji wa kipindi cha kwanza awamu ya tatu inaonesha mpango umechangia kwa kiasi kufikia azma ya serikali ya kupunguza umaskini nchini.

Alisema takwimu zinaonesha utekelezaji wa mpango kwa kipindi cha kwanza umechangiakupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi kwa kaya kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12 kwa kaya maskini sana nchini kote.

Pia alisema utekelezaji wa mpango umewezesha kaya za walengwa kujikita katika shughuli za kukuza kipato na kujiimarisha kiuchumi ikiwamo ufugaji, uvuvi, kilimo na biashara ndogo ndogo.





# Wanasiasa waonywa upotoshaji elimu bure

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANASIASA katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wametakiwa kuwa mstari wa mbele kuwashawishi wazazi kuchangia chakula cha mchana kwa ajili ya wanafunzi shuleni badala ya kuwapotosha wakitumia sera ya elimu bila malipo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega, wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Elimu wilayani hapa uliofanyika katika Shule ya Sekondari ya Rujewa na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa elimu.

Alisema baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiwapotosha wananchi kuhusu sera ya elimu bila malipo kwa kuwaambia kuwa hawatakiwi kuchangia chochote jambo ambalo alidai sio sahihi.

Mtega alisema ili kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi, kila mzazi anatakiwa kushiriki kwa kuhakikisha watoto wanakula chakula cha mchana wakiwa shuleni. Alisema jukumu la kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula shuleni ni la wazazi kwa kushirikiana na walimu na kwamba wazazi wanatakiwa kuwajibika kwa kuchangia chakula na walimu wanatakiwa kuhakikisha chakula kinapikwa.

"Sisi wanasiasa tuna wajibu mkubwa wa kuwafafanulia wananchi mambo yanayohusu sera mbalimbali. Sasa hivi kumekuwa na mivutano kwenye baadhi ya maeneo kuhusu uchangiaji wa chakula cha mchana kwa watoto wetu na baadhi ya wanasiasa wamekuwa chanzo cha upotoshaji," alisema Mtega.

Alisema ili kuinua kiwango cha elimu ndani ya wilaya, wazazi wanatakiwa kuhakikisha wanachangia chakula ili watoto wasome wakiwa na uhakika wa chakula.

Ofisa Elimu Sekondari wa Mkoa wa Mbeya, Majuto Njaga, alisema njia pekee ya kuinua kiwango cha ufaulu ni kuhakikisha kunakuwapo ushirikiano wa wadau wote wa elimu kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake.

Alisema wanafunzi wanapokuwa na uhakika wa chakula cha mchana, wanaongeza umakini kwenye masomo na kwamba hata kiwango cha utoro wa wanafunzi kinapungua. Njaga alisema serikali imekuwa ikiandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia sekta ya elimu na kwamba ili iwe na ufanisi ni lazima ifafanuliwe vizuri kwa wananchi ili wawe na uelewa wa kutosha.

"Mwalimu ni mlezi pia wa watoto lakini hawezi kutumia fedha zake kuwalisha watoto wetu, hivyo ni wajibu wetu wazazi kuhakikisha tunashirikiana na walimu kwenye malezi kwa kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wetu," alisema Njaga.

Naye Ofisa Elimu wa Wilaya ya Mbarali, Anna Shitindi, alisema wilaya inakabiliwa na matatizo mbalimbali kwenye sekta ya elimu ikiwamo upungufu wa vyumba vya madarasa, vyoo, madawati na nyumba za walimu.

Pia alisema wilaya hiyo inakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu jambo ambalo linasababisha wachache waliopo kuwa na mzigo mkubwa.



Wanafunzi wa Shule Msingi Makambini, Halmashauri ya Mji wa Tunduma, mkoani Songwe, wakisaidiana kubeba meza kupeleka kwenye moja ya ofisi za shule hiyo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kicheko kukamilika ujenzi wa barabara Chunya -Makongolosi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa barabara ya Chunya-Makongolosi mkoani Mbeya kwa kiwango cha lami, kutachochea shughuli za kiuchumi na kijamii katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi ikiwamo usafirishaji wa mazao na madini, imeelezwa.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Ibrahim Yoram, alisema hayo jana alipokuwa anazungumza na wandishi wa habari kuhusu maendeleo ya mradi wa barabara hiyo.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ambayo inajengwa na Mkandarasi Kampuni ya China Railway 15 Bureau Group Corporation umefikia asilimia 87 na kwamba barabara hiyo ina urefu wa Kilomita 39 kutoka Chunya mjini mpaka Makongolosi.

Kwa mujibu wa mkataba wa mradi huo, ujenzi wa barabara hiyo utakamilika Mei 31, mwaka huu, na kwamba kwa sasa shughuli zilizobakia ni umaliziaji wa baadhi ya maeneo yaliyobakia.

Meneja huyo alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi ambayo inajengwa kwa kutumia fedha za ndani na kwamba gharama ya mradi wote ni Sh. bilioni 59.7 na kwamba mpaka sasa, mkandarasi anaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 11.

"Hii barabara ni muhimu sana na ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara hii kwa awamu, lengo ni kuunganisha mikoa ya Mbeya na Tabora kwa kiwango cha lami. Tulianzia kipande cha Mbeya Chunya chenye urefu wa kilomita 72," alisema Yoram.

Alisema moja ya faida za barabara hiyo ni kurahisisha usafirishaji wa mazao na shughuli za madini katika Wilaya hiyo ambazo ndizo shughuli kuu za uchumi wilayani humo.

Pia alisema barabara hiyo ina madaraja makubwa matatu ambayo ndiyo yaliyochukua muda mrefu kwenye ujenzi na kwamba mpaka sasa ujenzi wa madaraja hayo likiwepo la Mto Lupa umefikia asilimia 96.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamriho, alifanya ziara ya kukagua wa mradi huo. Alimtaka mkandarasi wa barabara hiyo akamilishe mradi huo ndani ya muda uliopangwa.

Aidha aliridhishwa na kiwango cha ujenzi wa barabara hiyo pamoja na madaraja huku akiwataka maofisa wa TANROADS kuhakikisha wanafuatilia hatua kwa hatua ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa.

Alisema barabara hiyo ni muhimu na ni miongoni mwa malengo ya serikali kuhakikisha inaunganisha mikoa yote kwa barabara za lami ili kurahisha usafiri.

"Naombeni niwaagize mkandarasi mshauri na TANROADS, msimamieni huyu mkandarasi ili kuhakikisha anamaliza kazi hii ndani ya muda uliopangwa na wananchi waanze kunufaika na barabara hii," alisema Dk. Chamriho.

Hata hivyo aliahidi kuwa serikali itamlipa fedha zote mkandarasi huyo atakapokuwa amekamilisha kazi ya ujenzi wa mradi huo.

## Wanufaika TASAF wahimizwa miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali imewataka wanufaika wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini kuanzisha miradi itakayowasaidia baada ya mradi huo kufikia ukomo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, aliyasema hayo juzi alipowatembelea wanufaika wa mpango huo unaotekelezwa na Mfumo wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kijiji cha Mpakani, Kata ya Ubaruku na kuwaambia kuwa iko siku mradi huo utafika mwisho.

Mfune aliwataka wanufaika hao kuanzisha miradi ya ufugaji wa kuku, bata, samaki na shughuli za kilimo ambazo zitawasaidia kujiinua kiuchumi kama ilivyo lengo la mpango.

Alisema baadhi ya wanufaika wamekuwa wakizitumia fedha hizo kinyume na malengo ya serikali ikiwamo kunywea pombe na baadhi kuzitumia kwa kununua ngua na anasa zingine.

"Nimeona mwenyewe, wale ambao wameitumia vizuri fursa hii wanaonyesha mabadiliko makubwa. Nataka na wengine wote wawe hivyo kwani kuna watu nimepita wamefuga kuku, wamefuga nguruwe, bata na wengine walikuwa hawana uwezo wa kuwa hata na gunia moja la mpunga lakini leo wana mazao ya kutosha," alisema Mfune.

Alisema katika maeneo mengi ambayo alipita alibaini maendeleo makubwa kwa wanufaika na hivyo akawataka kujiendeleza ili baadaye waondolewe kwenye mradi na waingizwe watu wengine.

Mkuu huyo wa wilaya alisema miradi ya ufugaji wa kuku ni mizuri kutokana na gharama yake kuwa ndogo huku ikiwa na faida kubwa ikiwemo kuongeza ubora wa lishe kwa familia zao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpakani, Amos Mgongolwa alimwomba Mkuu wa Wilaya kuwatembelea mara kwa mara wanufaika wa mpango huo ili kubaini matatizo yanayowakabili na kuyatafutia ufumbuzi wa haraka.

Alisema katika kijiji hiocho kuna baadhi ya watu wanastahili kuingia kwenye mpango huo kutokana na hali zao za kiuchumi, hivyo akawaomba maofisa wa TASAF kufanya uhakiki kwa kuwaondoa walioinuka kiuchumi na kuwaingiza wengine.



# Waziri ajivunia maendeleo TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema wizara imeanza kupiga hatua katika kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika elimu.

Amesema pamoja na kuwapo changamoto kwa baadhi ya walimu wakuu katika kutumia teknolojia hiyo, bado wanapaswa kubadilika kwa kujifunza ili kwenda sambamba na wakati uliopo.

Waziri Simai aliyasema hayo jana katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Tunguu nje ya mji wa Zanzibar, wakati akikabidhi televisheni kwa baadhi ya walimu wakuu wa shule 15 za Unguja na Pemba kwa ajili ya kufundishia wanafunzi.

Alisema kutokana na upungufu wa walimu uliopo hasa katika masomo ya sayansi, kuna umuhimu wa kutumia teknolojia kwa kuwafundisha wanafunzi ili kupunguza tatizo hilo. Simai alisema wizara itaendelea kushirikiana na idara na taasisi zake ili kuwatafutia fursa pamoja na wadau mbalimbali kwa lengo la kuunganisha nguvu ili kutengeneza programu kwa faida ya taifa.

Pia aliwataka walimu wakuu hao kuhakikisha televisheni walizopatiwa ni za shule na zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kusisitiza kuwa TEHAMA inahitaji ujasiri na uvumilivu mzuri ili kufanikiwa. Ofisa Mdhamini Wizara ya Elimu Pemba, Mohammed Nassor Salim, aliipongeza SUZA na kushauri kukaa pamoja kujadiliana ili kutatua matatizo yaliyopo katika masuala ya matumizi ya TEHAMA kwa walimu wao.

Naye Makamu Mkuu wa SUZA, Dk. Haroun Ayoub Maalim, aliwataka wafanyakazi wa chuo hicho kuendelea kuandika miradi ili kunufaika zaidi na vifaa mbalimbali katika chuo chao, kama walivyofaidika kupitia mradi wa HUAWEI.

Akitoa maelezo kuhusu mradi uliosababisha kupata televisheni hizo, Mkuu wa Mradi wa kuandaa vipindi vya masomo ya Sekondari kwa Sayansi (HUAWEI) kutoka China, Dk Hassan Rashid Ali, alisema mradi huo umesaidia kuandaa vipindi ambavyo vilitumika kufundisha wakati shule zilipofungwa kutokana na mlipuko wa maradhi ya corona pamoja na kusaidia kwa shule mbalimbali Unguja na Pemba.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman akimkabidhi sadaka ya kumfariji Mzee Omar Abdallah Malik anayeishi Betras Shehia ya Sharifu Musa, Mkoa wa Mjini Unguja juzi, ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kujulia hali wagonjwa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jaji Mkuu ataka kasi utoaji uamuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, amewataka mahakimu wa wapya wa wilaya na mkoa kuongeza kasi ya kusikiliza kesi za matukio mbalimbali yakiwamo ya udhalilishaji wa kijinsia.

Makungu alisema hayo jana wakati akiwaapisha mahakimu wanane kwa ajili ya kuanza kazi kutokana na Tume ya Utumishi wa Mahakama kutoa kibali cha ajira.

Alisema Mahakama Kuu ya Zanzibar, tayari imeanzisha mahakama maalumu kwa ajili ya kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia ili kukomesha vitendo hivyo.

Jaji Mkuu alisema malalamiko mengi ya wananchi ikiwemo wazazi ni kuchelewa kusikilizwa kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia na kusababisha maumivu makubwa kwa waathirika.

"Tumeajiri Mahakimu wa Wilaya na Mkoa kwa lengo la kupunguza na kupambana na kesi za udhalilishaji wa kijinsia kuona zinasikilizwa haraka na kutolewa uamuzi," alisema.

Naye Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, Mohamed Ali Mohamed, alisema tayari mahakama maalumu kwa ajili ya kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia imeanza na kwamba kesi 160 zimepokewa na mbili kutolewa uamuzi huku 158 zikiendelea kusikilizwa.

Othman Ame Chum, Mrajisi wa Mahakama ya Kadhi, alisema ni matarajio yake makubwa kuona kesi nyingi zilizorundikana zikiwamo za utelekezaji wa wanawake na watoto pamoja na talaka zitapatiwa ufumbuzi haraka.

Alisema kesi za talaka na utelekezaji wa watoto ni changamoto kubwa inayoikabili mahakama ya kadhi ambayo awali imekabiliwa na tatizo la uhaba wa mahakimu.

"Tumepata mahakimu wawili kwa ajili ya mahakama ya kadhi ambao hawatoshi hata kidogo kutokana na wingi wa kesi hizo zinazopokewa mahakamani hapo," alisema.

## RC ataka ulinzi kuepusha vijana tabia hatarishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Masoud, amesema mkoa unakabiliana na changamoto zinazowakumba vijana kwa ajili ya kuwalinda na kuwanusuru kuepukana na tabia hatarishi.

Matter alisema hayo jana katika uzinduzi wa mradi wa elimu ya afya ya uzazi, virusi vya UKIMWI (VVU) na lishe kwa vijana balehe, uliofanyika katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake, Kisiwani humo.

Alisema serikali imekuwa ikandaa na kutekeleza mikakati ya kitaifa ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji, kuanzisha sera na mifumo ya elimu ya stadi za maisha na kushajiisha jamii katika ulinzi wa watoto.

"Katika kutekeleza mradi huu kwa ngazi za shehia, niziombe mamlaka za wilaya zote kuangalia mradi huu kama ni chachu ya maendeleo", alisema.

Mattar alisema katika mradi huo lazima kuwe na ushirikishwaji kwa taasisi zote ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na mradi huo ili kufikiwa malengo ya kuanzishwa kwake.

"Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza ndugu zetu wa jumuiya ya wanaoishi na virusi vya ukimwi (ZAPHA+) kwa umakini wao katika kusimamia malengo waliojiwekea, nikiri kwamba hakuna asietambua ZAPHA+ shughuli wanazozifanya kuisaidia jamii yetu hapa nchini", alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake Abdalla Rashid Ali, alisema, amefarijika kuweza kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Mwenyekiti wa Bodi ya ZAPHA+, Hasina Hamad Shehe, alisema ni vyema wadau na watakaohusika na mradi huo kutoa ushirikiano ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Akiwasilisha muhtasari wa mradi wa elimu ya afya ya uzazi, VVU na lishe kwa vijana balehe Zanzibar, Ofisa Miradi kutoka ZAPHA+, Salma Nassib, alisema mradi unalenga kuwafikia vijana 110,000 wenye umri kati ya miaka 10 hadi 19 kwa Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu ALLY ZAHARANI MOHAMED anatangaza kupotelewa na kadi ya Trailer aina ya SDC TRAILER yenye namba za usajili T 692 DSU.
Chassis namba SDCCS4583AAA64869.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa Polisi:
TAN/RB/191424/2021

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.100/2021**

Ombi la HAMIS MUNSHEHE PEMBE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu JUMA HAMIS MATUA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 11/05/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 13/04/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

RAMADHANI S. HAMIS anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 719 BAG – MERCEDES BENZ. Chassis namba WDC2030612R181590. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
WMB/RB/165/2021.

## TANGAZOLA KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA LIFEWORTH COMPANY LIMITED TUNAPENDA KUTOA TAARIFA KWA UMMA KUWA KAMPUNI HII YENYE NAMBA YA USAJILI No: 139079930 WA BRELA ILIYOPO MAENEO YA KIPAWA-ILALA DAR ES SALAAM INAYOJISHUGHULISHA NA UTOAJI WA MIKOPO MIDOGO MIDOGO, KATIKA KIKAO CHA WAKURUGENZI WOTE KILICHOFANYIKA TAREHE 02/01/2021 DAR ES SALAAM, WALIRIDHIA KUFUNGA KAMPUNI HII KWASABABU YA KUSHINDWA KUJIENDESHA YENYEWE.

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Waasi wachukua kambi ya kijeshi Myanmar

**Yangon,** MYANMAR

WAKATI maandamano dhidi ya utawala wa kijeshi yakiendelea nchini Myanmar, kundi la waasi limekiteka kituo cha kijeshi Mashariki mwa nchi hiyo, wakati mataifa ya Kusini mwa Asia yakisaka suluhisho la kisiasa.

Mapigano yalizuka kwenye eneo la Mashariki linalopakana na Thailand, ambako kundi la waasi wa jamii ya wachache ya Karen lilikivamia kituo kimoja cha kijeshi.

Mapambano yalikuwa makali tangu jeshi kunyakuwa madaraka Februari Mosi na kuiingiza Myanmar kwenye mzozo mkubwa wa kisiasa na kiusalama.

Karen National Union (KNU), moja ya makundi makongwe kabisa ya waasi nchini humo, lilisema lilikuwa limeichukuwa kambi hiyo ya kijeshi kwenye ukingo wa Magharibi wa Mto Salween, ambao unazitenganisha Myamnar na Thailand.

Wanavijiji walio upande wa Thailand waliripoti kusikia milio ya bunduki kabla ya jua kuchomoza hivi karibuni.

Picha za video zilizotumwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha moto na moshi kutokea kwenye eneo hilo lenye vilima na misitu.

Msemaji wa masuala ya nje ya kundi hilo, Saw Taw Nee, aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba vikosi vyao vilichukuwa udhibiti wa kambi hiyo majira ya saa kumi na moja alfajiri.

"Kambi nzima imechukuliwa na kuchomwa moto na sasa wapiganaji wetu wanatafuta maiti na majeruhi", alisema Saw akiongeza kwamba kulikuwa na mapigano kwenye maeneo mengine, ingawa hakueleza kwa undani zaidi.

Mapigano hayo yanatokezea wakati utawala wa kijeshi ukisema uko tayari kufikiria mapendekezo yaliyotolewa na Jumuiya ya Mataifa ya Kusini Mashariki mwa Asia (ASEAN) baada ya mkutano wa mwishoni mwa wiki nchini Indonesia.

Maelfu ya watu wamejitokeza mitaani katika maeneo mbalimbali ya nchi kwenye maandamano ya kuupinga utawala huo na kuonesha mshikamano wao na serikali kivuli inayoundwa na chama cha NLD kilichoondoshwa madarakani na kinachoongozwa na Aung San Suu Kyi.

**DW**

# Mtandao wazimwa Chad kudhibiti vurugu

**N'djamena,** CHAD

ANGA la Jiji la N'Djamena jana asubuhi lilijaa moshi wakati waandamanaji wakichoma matairi magurudumu na bendera za Ufaransa.

Kilio chao ni kufutwa kwa baraza la kijeshi la mpito.

Wanataka pia mazungumzo ya pamoja ambayo yanapaswa kusaidia kufanyika uchaguzi huru, wa haki na wazi wakati mamlaka ya kijeshi imechagua kutumia nguvu.

Watu kadhaa walisema waliona polisi wa kutuliza vurugu katika vitongoji vya jirani wakiingia katika nyumba kutafuta waandamanaji.

Mtandao ulizimwa ili kudhibiti upatikanaji wa taarifa na mvutano unaoongezeka unazidisha hofu kwamba Chad inaweza kuingia katika machafuko.

Nchi hiyo pia inakabiliwa na uvamizi wa waasi eneo la kaskazini, na kundi la waasi la Front for Alternation and Concord nchini Chad likipambana kupindua mamlaka ya kijeshi.

Waasi hao hivi karibuni limetaka kufanyika mazungumzo, takwa ambalo baraza tawala la kijeshi limekataa.

**BBC**



Wananchi wakiyahama makazi yao kufuatia majibizano ya risasi baina ya vikosi vya jeshi la Somalia na waasi, karibu na Wilaya ya Hodan jijini Mogadishu, juzi. **PICHA: REUTERS**

## Huawei yatumia TEHAMA kuinua Afrika katika uchumi wa kijani.

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

KAMPUNI ya teknolojia ya kimataifa, Huawei, imesema Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ina uwezo wa kupunguza uzalishaji wa kaboni kwa asilimia 20 katika muongo mmoja ujao.

William Xu, Mkurugenzi wa Bodi na Rais wa Taasisi ya Utafiti wa Mikakati wa Huawei, alisema uendelevu wa nishati ni changamoto kubwa ambayo itazikabili nchi zote.

"Matumizi ya nishati ulimwenguni yanaongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.7 kila mwaka. Hivi sasa asilimia 85 ya nishati hutokana mabaki ya mimea na wanyama wa kihistoria yaani."

"Uendelevu wa nishati hii ni changamoto kubwa inayotukabili sisi sote. Kwa kuwezesha sekta mbalimbali, TEHAMA ina uwezo wa kupunguza uzalishaji wa kaboni ulimwenguni kwa asilimia 20 katika muongo mmoja ujao," Xu alisema.

"Kwa matumizi ya nishati, lazima tupendekeze mifumo jumuishi ya nishati kwa majumbani na viwandani na kuunda jamii, vyuo na miji isiyozalisha kaboni." alisema Xu.

Hivi karibuni, Huawei ilitangaza kuwa itazingatia ubunifu na teknolojia mpya kusaidia viwanda kupunguza matumizi ya nishati, ili kupunguza uzalishaji wa kaboni duniani.

Barani Afrika pia, nchi nyingi zinazidi kuhamia katika matumizi ya nishati mbadala ili kusonga mbele katika nishati endelevu kwa siku zijazo na Huawei imetoa zaidi ya mifano ya gridi 200 ya umeme kwa nchi zaidi ya 30.

Katika umeme wa jua pekee, Afrika imepata maendeleo makubwa katika miaka ya hivi karibuni.

Zaidi ya gridi 6,200 ambazo hujumuisha gridi za biashara na viwanda pamoja na zile ndogo zimethibitishwa kuwapo barani humo.

Huang Su, Mkurugenzi wa Huawei katika Biashara ya Umeme Dijitali Kusini mwa Afrika, alisema kwamba karibu nusu ya idadi ya watu wasio na uwezo wa kupata umeme duniani, wanaishi Kusini mwa jangwa la Sahara.

"Kwa hivyo kuna haja kubwa na ya dharura ya kuharakisha ukuaji wa nishati mbadala kote katika eneo hilo ili kuhakikisha nishati ya kutosha, nafuu na ya kuaminika kwa Waafrika wote na kwa nchi kupata faida ya uchumi wa kijani." alisema.

Huawei imetumia zaidi ya miaka 30 ya utaalam na uzoefu katika teknolojia ya kidijitali ili kufanya uzalishaji wa umeme wa jua na matumizi kuwa bora zaidi na ya kuaminika kwa gharama ndogo.

## Hofu yazuka Mogadishu baada mapigano

**Hodan,** SOMALIA

HOFU imezuka Mogadishu baada ya watu kuanza kutoroka makazi yao katika Wilaya za Hodan na Hawlwadag, kufuatia kuongezeka kwa operesheni za kijeshi kati ya serikali na vikosi vya upinzani katika vitongoji hivyo. Barabara za jiji zilijaa magari wakati familia kadhaa zikipakia bidhaa na mali zao, ili kutorokea maeneo yaliyo salama.

Watu walianza kuyakimbia maeneo hayo baada ya vikosi vya upinzani kuhamia mtaa wa Siigaale wa wilaya ya Hodan.

Kikosi maalum cha polisi wa Haramad pia kilifika katika maeneo hayo mapema leo asubuhi ili kuchukua nafasi ya wapiganaji wa upinzani walioondoka.

Wakati huo huo, Marekani ilionesha wasiwasi juu ya mapigano makali huko Mogadishu, ikihimiza pande husika kuanza tena mazungumzo.

Washington ilisema iko tayari kuzingatia vikwazo ili kuzuia juhudi za kudhoofisha amani na utulivu nchini Somalia.

Kwa upande mwingine, polisi waliopewa mafunzo na Uturuki huko Gorgor walivamia Redio ya Mustaqbal, wakampiga mwandishi wake wa habari na kuchukua vifaa.

Hiki ni kisa cha hivi karibuni kwa waandishi wa habari kuvamiwa kwa kutangaza kuhusu ghasia nchini humo.

# Aguero ataka kujiunga Barca



**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Sergio Aguero, amewaambia watu wake wa karibu juu ya kutaka kujiunga na Klabu ya Barcelona kule nchini Hispania.

Kwa sasa inajulikana wazi kwamba, mshambuliaji huyo wa Argentina, hatakuwa kwenye kikosi hicho baada ya msimu huu kumalizika kwa kuwa hatoongezewa mkataba mwingine na kikosi hicho.

Taarifa zinasema kuwa nyota huyo, Aguero ambaye alicheza ndani ya LaLiga akiitumikia klabu ya Atletico Madrid, kwa sasa anahitaji kurejea tena kwenye ligi hiyo.

Aguero, mwenye umri wa miaka 32, amekuwa akisemekana kujiunga Chelsea pamoja na Manchester United ambazo zinamhitaji kumuona nyota huyo akibaki ndani ya Ligi Kuu England.

Lakini kwa mujibu wa watu wake wa karibu walionukuliwa na gazeti la Marca la nchini Hispania, Aguero anataka kwenda Barcelona.

Ikimbukwe kuwa Aguero ni rafiki mkubwa zaidi wa Lionel Messi, nahodha wa Barcelona ambaye anatajwa kuwashawishi mabosi wa timu hiyo ya Catalunya kumsajili nyota huyo, ambaye ni mfungaji wa wakati wote pale kwenye dimba la Etihad.

# Rodgers atajwa Spurs



**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur, inaonekana kumhitaji Brendan Rodgers akachukue mikoba ya kuinoa timu hiyo katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, ameendelea kufanya kazi ya ziada akishirikiana na wataalamu wake kumtafuta mbadala wa Jose Mourinho na kocha huyo wa Leicester ndio anaonekana kuwa chaguo la kwanza.

Ikiwa saini ya Rodgers itakuwa ngumu kupatikana, Spurs inatarajiwa kuangukia kwa kocha wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, ambaye pia anawindwa na Bayern Munich.

Hii si mara ya kwanza kwa Spurs kuonyesha nia ya kuhitaji kumsainisha Rodgers, kwani iliwahi kujaribu suala hilo mwaka 2012 wakati anaifundisha Swansea.

Rodgers aliitosa Spurs kwa sababu alipata ofa nono kutoka Liverpool ambayo baadaye ilimfungashia virago na kumchukua, Jurgen Klopp.

Baada ya kuondoka Liverpool alijiunga na Celtic ambayo aliiwezesha kushinda mataji saba ya michuano ya ndani kisha akatimkia zake Leicester City, Februari 2019.

Leicester kwa sasa ipo nafasi nzuri ya kumaliza kwenye nne bora katika msimamo wa ligi na imeingia fainali ya FA kwa mara ya kwanza baada ya miaka 51.

# Bailly apewa mkataba mpya



**MANCHESTER,** England

ERIC Bailly amesaini mkataba mpya na Manchester United utakaombakisha klabuni hapo hadi Juni mwaka 2024.

Mkataba wake wa sasa wa Bailly ulikuwa umalizike mwishoni mwa msimu ujao, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amekubali kuongeza muda wa kukaa huko Old Trafford.

Beki huyo wa kati wa Ivory Coast ambaye katika mkataba wake kuna kipengele kinachomruhusu kuongeza mwaka mmoja zaidi, amecheza michezo 15 kwa United, lakini amekuwa akikabiliwa na majeraha mara kwa mara.

"Nina furaha sana, uamuzi huu ni kitu ambacho hata nilikuwa sijafikiria, naipenda klabu hii na ninapenda kuichezea Manchester United," alisema Bailly.

"Kila kitu kipo vizuri sasa kipindi cha majeraha kimepita nipo sawa na najihisi vizuri hivyo tu."

Bailly alijiunga na Man United akitokea Villarreal kwa ada ya pauni milioni 30 mwaka 2016.

## HABARI MICHEZO

# Ibrahimovic mikononi mwa sheria kwa kubeti



**MILN,** Italia

NYOTA wa AC Milan na timu ya Taifa ya Sweden, Zlatan Ibrahimovic, ameingia kwenye mikono ya sheria, kwa madai ya kujihusisha na michezo ya kubashiri.

Ibrahimovic anafanyiwa uchunguzi na kamati ya maadili ya Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa) kwa kile kilichoripotiwa kuwa mchezaji huyo anajihusisha na masuala ya michezo ya kubashiri maarufu kama 'kubeti'.

Kwa mujibu ya sheria za Uefa, ni marufuku kwa mchezaji yeyote kujihusisha na masuala ya kubashiri michezo.

Ibrahimovic, ametajwa kuingia ubia na kampuni inayojihusisha na michezo ya kubashiri na hivyo kuingia kwenye mikono ya sheria kwa kuvunja sheria za Uefa.

Taarifa ambayo imetolewa nchini Sweden kama ambavyo imechapishwa na Uefa imesema; "Ofisa upelelezi wa maadili na nidhamu wa Uefa, ameteuliwa leo kuanza uchunguzi wa kinidhamu kuhusu kuvunjwa kwa taratibu za kinidhamu za Uefa ambapo kumefanywa na Zlatan Ibrahimovic ambaye anahusishwa kuwa na ubia na kampuni ya kubashiri."

Hii ni mara ya pili kwa Ibrahimovich kuingia kwenye mikono ya sheria msimu huu.

Itakumbukwa kwenye mchezo wa Coppa Italia dhidi ya Inter Milan, aliingia kwenye ugomvi na Romelu Lukaku ambapo mzozo huo uliwafanya wote wawili kupigwa faini.

# Sima azigonganisha Man United, Arsenal




**LONDON,** England

TIMU za Manchester United na Arsenal zipo kwenye mbio moja ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Slavia Prague, Abdallah Sima.

Sima mwenye umri wa miaka 19, amekuwa na msimu bora ambapo amefunga jumla ya mabao 19 kwenye mashindano yote yakiwamo manne kwenye Ligi ya Europa.

Arsenal inayonolewa na kocha Mikel Arteta, ndiyo ilikuwa ya kwanza kuwania saini ya Msenegal huyo.

Lakini sasa BT Sport imeripoti kuwa Man United nayo imejitosa kwenye mbio za kuwania saini ya straika huyo kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kipindi cha majira ya joto.

Pia amehusishwa kujiunga na West Ham United ambao imeelezwa kuwa wanamfuatilia kijana huyo.

Sima ana uwezo wa kucheza upande wa kulia na kati na ana uwezo wa kutokea upande wowote katika kushambulia jambo ambalo linatajwa kuwavutia mabosi wa Old Trafford.

Mchezaji wa zamani wa Klabu ya Slavia Prague, ambaye ni kiungo, Tomas Soucek anayekipiga ndani ya West Ham amesema: "Ninaweza kusema kwamba watu wa West Ham wanamtambua kijana. Ninapenda kuona kwamba mchezaji mwingine kutoka Slavia anakuja hapa ila ni safari ndefu.

"Bado ni mchezaji kijana na anaweza kuonyesha kwamba anaweza. Wengi wanajua kuhusu yeye na hilo si jambo baya kwake."

# Iheanacho atabiriwa makubwa Leicester



**LONDON,** England

NYOTA wa Leicester City, Kelech Iheanacho, ametabiriwa na Jamie Carragher atakuwa mfungaji wa kutegemewa wa timu hiyo kama ilivyo kwa Jamie Vardy.

Iheanacho amekuwa mchezaji muhimu wa Leicester katika mechi za hivi karibuni, na tayari amefanikiwa kufunga kwenye mabao 14 msimu huu katika mashindano yote.

Mwishoni mwa wiki, Iheanacho alifunga goli lililoisaidia Leicester kutinga fainali ya FA ambapo sasa watakutana na Chelsea baadaye mwezi ujao.

Mchezaji huyo wa Nigeria kabla ya mechi hiyo alifanikiwa kuvunja rekodi yake mwenyewe ya kuwa Mnigeria wa kwanza kufunga mabao mengi (9) katika Ligi Kuu ya England.

Na sasa Carragher anaona kwamba, Iheanacho anaweza kuwa mfungaji bora zaidi kwa kikosi hicho.

"Naweza kusema ni Vardy wa baadaye," alisema Garragher akinukuliwa na BT Sport.

"Kipaji chake ni kikubwa na uwezo wake uwanjani ni wa kuvutiwa, huwa nafurahia sana kumtazama akicheza," alisema.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AANZA KUULIZIA SOKA LA ENGLAND, HISPANIA

Anaulizia kuhusu mchezo ukoje na tamaduni zao zikoje pale na kila siku anatazama...

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, amesema nyota, Kylian Mbappe anaulizia kuhusu England na Hispania wakati huu uvumi ukitawala kuhusu majaliwa yake.

Mbappe amekuwa akihusishwa sana na mpango wa kuhamia kwa mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid, na awali kwa bingwa mtetezi wa Ligi Kuu England, Liverpool.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, mkataba wake unamalizika mwaka 2022, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG bado wana matumaini ya kumsainisha mkataba mpya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

**Pochettino aliulizwa kuhusu uhusiano wake na Mbappe kuelekea mchezo wa leo Jumatano wa nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City.**

"Kylian anapenda soka, anapenda kuzungumzia kuhusu soka," alisema Pochettino.

"Anaulizia kuhusu England - mchezo ukoje, tamaduni zao zikoje pale? Na pia anaulizia kuhusu Hispania na Argentina.

"Anatazama kila siku mechi za England, Ufaransa, Italia na Ujerumani.

"Ndio kwanza ana umri wa miaka 22, lakini amepevuka sana, anajiamini kuhusu kipaji chake.

"Anazungumza Kifaransa, lakini pia anapendelea Kiingereza na Kihispania.

"Nazungumza naye Kiingereza na Kihispania, mara nyingi zaidi Kiingereza kuliko Kihispania.

"Siku moja nilimwambia: 'Nahitaji kujifunza zaidi Kifaransa kupitia wewe, niimarike zaidi', na alisema: 'sawa, lakini kwangu mimi napenda kuzungumza Kiingereza'. Anapenda kujifunza lugha mbalimbali.

"Kabla ya mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona, nilimwambia mimi nimeshinda pale mara moja tu nikiwa na Espanyol na akasema kwa umakini mkubwa: 'sawa, kesho itakuwa ni mara ya pili kwako'.

"Nikamwambia: 'Unauhakika?' Na akasema: 'ndio usihofu. Tunakwenda kushinda'. Alikuwa anacheka mara baada ya mchezo na aliniambia akiwa uwanjani: 'Nilikwambia, nilikwambia, nilikwambia'."

## KWA UFUPI

### PSG WANAONGOZA KWA RONALDO

KLABU ya Paris St-Germain wapo mbele ya Manchester United katika mpango wao wa kumsajili mshambuliaji nyota wa Ureno na Juventus, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36. (***Tuttosport***)

### MORAN AWINDWA ENGLAND

CHELSEA na Manchester United wanamuwinda kiungo kinda wa Brighton, Andrew Moran mwenye umri wa miaka 17. (***Team Talk***)

### BARCA UHAKIKA KWA GARCIA

BARCELONA wana imani kuwa Eric Garcia mwenye umri wa miaka 20, atajiunga na klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu, baada ya mkataba wa beki huyo na klabu yake ya Manchester City utakapomalizika. (***Mundo Deportivo***)

### SIMA AWINDWA UNITED

MANCHESTER United wanamuwinda mshambuliaji wa klabu ya Slavia Prague, Abdallah Sima mwenye umri wa miaka 21. (***Manchester Evening News***)

### RD WATAKA DAU NONO

RB Leipzig wanataka dau litakalovunja rekodi ya usajili wa makocha la euro milioni 25 kutoka Bayern Munich ili kumuachia kocha wao, Julian Nagelsmann. (***Sky Sports***)

### SPURS WAMTAKA HAG

KLABU ya Tottenham Hotspur, sasa itaelekeza nguvu kumsajili kocha wa Ajax, Eric ten Hag, wakati huu ambapo Bayern inaonekana ipo mbioni kumsajili Julian Nagelsmann. (***Telegraph***)

### ARSENAL KUMBAKIZA ROWE

ARSENAL wameanzisha mazungumzo na kiungo wao kinda, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 20, ili kumpatia mkataba mpya. (***The Athletic***)

### DONNARUMMA KUBAKI MILAN

GOLIKIPA wa Italia, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 22, atasalia katika Klabu ya AC Milan licha ya mkataba wake kuisha mwishoni mwa msimu huu na kutakiwa na Klabu za Manchester United na Chelsea. (***TalkSport***)

### MADRID KUMUACHIA VARANE

REAL Madrid hawatakaza msuli kumbakisha klabuni hapo beki wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akiwaniwa na Manchester United na Chelsea. (***AS***)

### SHAQIRI KUONDOKA LIVERPOOL

KIUNGO wa Uswizi, Xherdan Shaqiri mwenye umri wa miaka 29, anataka kuondoka Liverpool mwishoni mwa msimu ili kupata sehemu atakayocheza zaidi. (***Football Insider***)

### WANNE KUUZWA ARSENAL

ARSENAL ipo tayari kuwauza wachezaji wanne mwishoni mwa msimu ili wapate fedha za kufanya usajili mpya. (***Football London***)

HABARI MICHEZO

# OPPA WA SIMBA APANIA KIATU CHA DHAHABU WPL

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba Queens, Oppa Clement, amesema msimu huu anataka kuutumia kufuta ufalme wa nyota wa JKT Queens, Fatuma Mustapha, ambaye amekuwa mfungaji bora kwa misimu yote ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara (WPL) tangu ianzishwe.

Oppa ambaye kwa sasa ni kinara wa mabao katika ligi hiyo, baada ya kutikisa nyavu mara 25, amewacha hatua tano zaidi Fatuma katika orodha ya wafungaji wanaowania Kiatu cha Dhahabu WPL.

Akizungumza na gazeti hili jana, Oppa alisema amejipanga kupambania nafasi ya ufungaji bora, lakini kubwa zaidi kwake atafurahi kuona timu yake inachukuwa ubingwa kwa mara ya pili mfululizo. Alisema dhamira yao kubwa tangu kuanza kwa msimu huu ni kuhakikisha wanatetea ubingwa wao, hivyo ana imani watafikia hilo, lakini pia kupambana katika vita vya kuwania tuzo ya ufungaji bora.

> **"Malengo yetu kama wachezaji ni kuona Simba inatwaa ubingwa, hilo linawezekana, kwa sababu tuko vi zuri, hivyo ni ku hakikisha tunapam bana kutafuta pointi muhimu katika kila mechi, ili kufikia malengo hayo.**

"Kuhusu tuzo ya ufungaji bora, nina imani ni kazi kubwa kutokana na wachezaji wengi kuzidiana mabao machache, ila msimu huu nimejipanga kubeba tuzo mbili ikiwamo ufungaji bora na kuipa Simba ubingwa," alisema Oppa.

Alisema ili malengo yao yatimie ikiwamo ufungaji bora, ni kuhakikisha kila mechi anayopata nafasi anazitumia vizuri kufunga zaidi ya bao 1 na kuendelea ili kujiimarisha kwenye tuzo hiyo.

TUNAWAFUATA...




Wachezaji wa Yanga, kiungo Haruna Niyonzima (Kushoto) na mshambuliaji Ditram Nchimbi, wakielekea kupanda 'pipa' kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam tayari kwa safari ya kwenda kuivaa Tanzania Prisons katika mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa. **MPGAPICHA WETU**

# Polisi yaipiga mkwara Azam FC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuichapa Mtibwa Sugar mabao 2-1 juzi, kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, klabu ya Polisi Tanzania imeipiga mkwara Azam FC kuelekea kwenye mechi ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya ushindi huo, Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Robert Munishi, amesema ana hamu ya kukutana na Azam ili walipe kisasi cha kufungwa bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu.

Pamoja na kwamba Azam imeonekana kuwa tishio kwa siku za karibuni, hasa baada ya kuichapa Yanga bao 1-0 Jumapili iliyopita, Munishi alisema hilo haliwasumbui.

"Azam huwa tunawakamata sana, ila dakika za mwisho ndiyo wanatufunga, sasa safari hii tunahamu nao ili tuwaonyeshe tena huko huko kwenye uwanja wao mzuri,'" alisema Makamu Mwenyekiti huyo.

Kuhusu suala hilo la uwanja, Munishi alisema wao ni kama Simba, falsafa yao ni mpra wa chini na pasi fupi fupi, hivyo wanapokutana na timu kwenye uwanja mzuri, na wao wanacheza vema na ndiyo maana hawakushinda mechi zao mbili za nyumbani, lakini wakashinda ugenini mabao 2-1 dhidi ya Mtibwa.

"Unaona tulifungwa mabao 2-1 nyumbani dhidi ya Prisons, halafu mechi iliyofuata tunafungwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City nyumbani, ni kwa sababu uwanja wetu haukuwa rafiki, ulikuwa na maji na matope mengi, lakini kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro tumeukuta uko vizuri, tumeshinda.

"Pamoja na kwamba tunautumia Uwanja wa Chuo cha Ushirika kuwa wa nyumbani, lakini unamilikiwa na chuo si wetu, hatuumiliki moja kwa moja kwa hiyo ni changamoto kidogo," alisema.

Kwenye Ligi Kuu, Polisi Tanzania inakamata nafasi ya nane kwa pointi 37 ilizonazo baada ya kushuka dimbani mara 28 kama ilivyo kwa Azam FC inayoshika nafasi ya tatu kwa alama zake 54.

## BIASHARA YAFUNGUKA KICHAPO CHA KAGERA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Marwa Chamberi amesema mfumo waliotumia kuifunga Kagera Sugar ambayo inafundishwa na kocha wa zamani wa timu hiyo, Francis Baraza, ni ule ule ambao yeye alikuwa anaufundisha zamani.

Kocha huyo alisema hayo baada ya Biashara United kuitungua Kagera Sugar mabao 2-1 juzi kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume, Musoma mkoani Mara, huku Baraza kwa mara ya kwanza akicheza dhidi ya timu yake ya zamani.

Chamberi alisema kuwa Baraza alitengeneza mfumo mzuri wa uchezaji kwenye timu ya Biashara ambayo si rahisi sana kuubadilisha kwani imekuwa ni kama falsafa ya timu, na kwa bahati mbaya kwake au nzuri kwao, mfuno huo ndiyo umemuangamiza.

"Nilibadilisha vitu vidogo sana, lakini mfumo ni ule ule wa Baraza ndiyo niliotumia, mpaka leo bado namheshimu kocha huyo kwa sababu ameweka msingi mzuri wa uchezaji kwenye timu yetu ndiyo maana kwa asilimia kubwa sikubadilisha vitu vyote, ni vichache tu," alisema Chamberi.

## TAIFA UFUKWENI SASA YATAFUTIWA 'WAKUITESTI'

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limesema limeshapeleka maombi katika mataifa mbalimbali ikiwamo Senegal, Cape Verde na Morocco, ya kupata mechi za kujipima nguvu dhidi ya timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni inayoenda kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika, zitakafanyika nchini Senegal Mei 23-29, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Afisa Habari wa Shirikisho hilo, Clifford Ndimbo, alisema walipokea maombi ya kocha wa timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawassa, kuhitaji kupata mechi za kujipima nguvu wa kikosi cha timu hiyo na tayari wameanza kuyafanyia kazi.

Alisema wamepeleka maombi na sasa wanasubiri majibu ili kuhakikisha wanapata mechi hizo haraka kutokana na muda kutokuwa rafiki kulingana na mashindano kutarajiwa kuanza mwezi ujao.

"Tayari tumeomba mechi katika hizo nchini na nyingine, kwa sasa tunasubiri majibu ikiwamo wenyeji wa mashindano hayo, ila siku za mechi bado hazijajulikana kwa sababu hatujapata majibu kamili kutoka kwa wenzetu tuliowaomba kuja kucheza nao," alisema Ndimbo.

# Michezo

Jumatano Aprili 28, 2021

Nipashe




HABARI UK.22

## Mbappe aanza kuulizia soka la England, Hispania

## Nabi atoa mkakati Yanga kwa Prisons

**Na Saada Akida**

HUKU ikiwa na matarajio makubwa ya kuibuka na ushindi kesho katika mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, ugenini dhidi ya Tanzania Prisons, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameanza na safu ya ushambuliaji kutokana na kukosa umakini wa kutumia nafasi wanazotengeneza.

Nabi alitoka kichwa chini Jumamosi iliyopita katika mechi ya kwanza kuiongoza timu hiyo kwenye Ligi Kuu Bara baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Azam FC, mchezo ukipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa mujibu wa kocha wa makipa wa Yanga, Razak Siwa, alisema Nabi amewaambia wachezaji wake anataka soka la kushambulia na washambuliaji kuongeza umakini na utulivu wanapopata nafasi uwanjani.

Alisema mbali na ushambuliaji, pia amewataka nyota wake kuziba nafasi na mara timu inapopoteza mpira, kujipanga kwa haraka katika ukabaji huku akiwasisitiza kuonyesha nidhamu kwa mpinzani wao.

"Kitendo cha kupoteza mechi yake ya kwanza hakupendezewa nacho, amewaambia hataki soka la kubutua butua na kila mmoja apambane kwa maslahi ya timu ili kufikia malengo yao.

"Sasa kila mchezaji amepewa majukumu yake ya kuhakikisha tunaenda kufanya vizuri kwenye mechi ijayo ya FA, hasa umakini kwa safu ya ushambuliaji kwa kutumia vema nafasi wanazotengeneza uwanjani," alisema Siwa.

Yanga kesho itashuka Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa kuvaana na wenyeji, Tanzania Prisons kwenye mechi ya robo fainali Kombe la FA.

**LA MOTO...**



Beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akiachia shuti kali lililozama kimyani na kuiandikia timu yake bao pekee wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Gwambina FC Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Gwambina. PICHA: SIMBA. **PICHA: SIMBA**

# TSHABALALA AWEKWA SOKONI SH. MILIONI 392

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Yanga yakaribishwa kuchuana na Mamelodi na Kaizer Chiefs, hiyo ikiwa ni thamani yake kwa mkataba wa miaka...

WAKATI beki wa pembeni wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akiwa amebakiza miezi miwili kabla ya mkataba wake na Simba kumalizika, huku akihusishwa na kusajiliwa na Yanga, Meneja wake, Herry Mzozo, ametangaza dau linalotakiwa ili kuipata huduma ya mchezaji huyo.

Tshabalala ambaye pia anajulikana kwa jina la Zimbwe Jr, amekuwa katika kiwango cha juu kwa sasa, na tayari klabu kadhaa zikiwamo za nje zimeanza kuitolea macho huduma yake baada ya kufahamika kuwa hajafanya mazungumzo yoyote na klabu yake mama, Simba.

Hata hivyo, Meneja wa mchezaji huyo, Mzozo, amesema taarifa za Tshabalala kutakiwa na Yanga, hizo ni tetesi tu na kwamba klabu hiyo haijatoa ofa yoyote, ila kama wanamtaka basi dau la kumsajili ni Sh. milioni 200 kwa mkataba wa miaka miwili huku mshahara wake ukiwa ni Sh. milioni nane kwa mwezi.

Hiyo ikiwa na maana kwamba, kama timu hiyo itafanikiwa kumsajili, kwa kipindi cha miaka miwili, italazimika kumlipa Sh. milioni 192 kama mshahara pekee, hivyo jumla pamaja na hela ya usajili atakunja Sh. milioni 392.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Mzozo alisema Klabu ya Kaizer Chief na Mamelodi Sundowns za Afrika Kusini ni miongoni mwa zilizoonyesha nia ya kuhitaji huduma ya Tshabalala ambaye amekuwa katika kiwango cha juu msimu huu.

"Kwa sasa amebakiza miezi miwili katika mkataba wake na kama Yanga wanamtaka walete milioni 100 kama ada ya usajili kwa kipindi cha mwaka mmoja na mshahara wake ni Sh. milioni 10 hadi nane.

"Kwa sasa tunasubiria mkataba na Simba uishe, tufanye uamuzi wetu mwingine, kama kweli wangetuhitaji tungelimaliza ndani ya miezi sita kama walivyofanya kwa wachezaji wengine," alisema Mzozo

Alisema mazungumzo ya awali kati yao na mtu aliyetumwa na Simba hawakuelewana, hivyo kwa sasa kuna ofa mezani kutoka timu hizo kubwa za Afrika Kusini, mshahara wake ukitarajiwa kuwa Sh. milioni 23 kwa mwezi.

Kuhusu Yanga, Mzozo aliongeza: "Mambo ya Yanga nasikia sikia tu watu wanaanzisha wenyewe na kujijibu wenyewe. Hapa uswahilini kwangu sijaona Yanga wakinifuata lakini hata hivyo kama Yanga wanataka kutufuata si dhambi."

Hata hivyo, uongozi wa Simba kupitia kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Barbara Gonzalez, amesema kwa sasa wanaelekeza nguvu kwanza kwenye kutetea ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Tshabalala ametoa mchango mkubwa kwa Simba kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kutinga hatua kama hiyo kwenye Kombe la FA nchini pamoja na kuongoza msimamo wa Ligi Kuu Bara wakati huu wakiwania kutetea taji hilo kwa mara ya nne mfululizo.

Simba ambayo jana iliikaribisha Dodoma Jiji kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, keshokutwa, Ijumaa itajua timu itakayokutana nayo kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati droo itakapofanyika jijini Cairo, Misri.

Timu ambazo Simba inaweza kukutana nazo katika hatua hiyo ni Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, MC Alger ama CR Belouizdad za Algeria.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042